**8 SEPTEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Tisa – Tarehe 8 Septemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma kwa Kipindi cha tarehe 1 Julai, 2021 hadi 30 Juni, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 122

### *GGML* ku-*blacklist* vijana nchini

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, Serikali inatambua utaratibu wa Mgodi wa *GGML* wa ku-*blacklist* vijana nchini na ni vijana wangapi wapo *blacklisted*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imewahi kupata malalamiko kuhusu Mgodi wa *GGML* ku-*blacklist* vijana ambao wamesitishiwa ajira zao na Mgodi huo kwa sababu mbalimbali. Ufuatiliaji uliofanyika haukubaini suala hili. Kilichobainika ni kuwa mgodi umeweka utaratibu wa kutunza taarifa za kiutendaji na mienendo ya wafanyakazi wake ikiwemo matendo/matukio ya ukiukwaji wa kanuni na taratibu ambayo mfanyakazi anakuwa amefanya katika kipindi cha ajira yake.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kuajiri, Kampuni/Waajiri karibu wote hufuatilia taarifa za utendaji wa waombaji wa kazi kwa waajiri wao wa awali. Hivyo, *GGML* imekuwa ikitoa taarifa za utendaji na mienendo ya wafanyakazi waliowahi kufanya kazi nao pale inapoombwa kufanya hivyo. Aidha, pamoja na kutoa taarifa hizo, *GGML* haizuii kwa namna yoyote Mgodi husika kuwaajiri waombaji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwataka vijana ambao wana uhakika utumishi wao katika Mgodi wa *GGML* haukuwa na dosari na wanaweza kuthibitisha kuwa wamekuwa *black-listed* katika kampuni hiyo kuwasiliana na Ofisi yangu ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Aidha, nichukue nafasi hii kuwasihi vijana wote kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu ili kujiepusha na athari za kuwa kwenye kumbukumbu mbaya za utumishi wao hali inayokwamisha jitihada zao za kujikwamua kiuchumi na kushiriki katika Ujenzi wa Taifa letu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa upo ushahidi kwamba hiki kinachoitwa taarifa kimekuwa kikitumika na kinaendelea kutumika kuwanyima haki Watanzania ambao hata kama walikutwa na tatizo dogo tu, kufanya kazi katika migodi yote mikubwa Tanzania. Serikali ipo tayari kulitolea maelekezo?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa taarifa hizi ambazo zimeitwa taarifa, naita *blacklisting*, zinapomkuta Mtanzania zinadumu milele kinyume na Sheria ya Makosa ya Jinai. Mtu anapotuhumiwa anaadhibiwa na baadaye anakuwa Mtanzania huru.

Je, Serikali ipo tayari kutoa maelekezo ili makosa haya yasiwaadhibu Watanzania milele, wasiajiriwe popote pale katika migodi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Kanyasu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza la kuhusiana na kwamba anao ushahidi wa matendo haya kutokea. Namuomba Mheshimiwa Mbunge Constantine Kanyasu, anipatie ushahidi huo kama tulivyoahidi kwenye majibu yangu ya msingi ili tuweze kuhakikisha haki za Watanzania hawa zinatendeka kwa sababu, Serikali ni wajibu wetu kulinda pande zote na sisi ndiyo wasimamizi na *custodian* wa sheria lakini pia usimamizi wa Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, ni kinyume kama kweli itakapoonekana ushahidi upo, unaothibitisha kwamba hao watu wametendewa kinyume na kutumia *arbitrariness procedures* ambazo na pengine wakati mwingine *discretional powers* ambazo waajiri wao wanakuwa wanazitumia kuwagandamiza Watanzania. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, nipate orodha hiyo, na mimi na yeye tutafanya kazi hiyo na ninamuahidi tutafika kwenye mgodi husika ambao ameulalamikia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kosa kuwa milele. Ni *principle* yetu kwamba mtu atatuhumiwa lakini pia utaratibu utafanyika wa kuthibitisha kosa hilo. Kama ni la jinai, itakuwa *beyond reasonable doubt* na kama ni kosa la dawa, itakuwa ni *on balance of probability*. Sasa yale ambayo yamethibitika *beyond reasonable doubt* na hatua zikachukuliwa, maana yake ukishatoa adhabu, haihesabu tena kosa hilo kuja kutumika.

Mheshimiwa Spika, ni kosa kisheria kufanya hivyo, hilo nalo pia ninalichukua na nampongeza Mheshimiwa Mbunge kama amebaini hayo ili tuwatendee haki Watanzania ambao lazima washiriki katika ujenzi wa Taifa lao na kufanya kazi kwa ajili ya nchi hii, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa sasa aulize swali lake.

Na. 123

**Uhaba wa watumishi Wilayani Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha Wilayani Ludewa hususan eneo la elimu, afya na uvuvi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ikama ya mwaka 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inahitaji jumla ya watumishi 3,327. Watumishi waliopo ni 1,985 hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 1,342 sawa na asilimia 40.33.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali iliajiri jumla ya wataalam 149 wa kada za afya, elimu msingi, sekondari na

uvuvi na kuwapangia Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. Serikali inatambua upungufu huo wa watumishi na itaendelea kuajiri wataalam wa kada mbalimbali na kuwapanga kwenye maeneo yenye mahitaji kote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida ya Serikali kuwapangia watumishi Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na kuwahamisha kabla hawajaripoti hasa madaktari, je, nini mpango wa Serikali kutoa ajira mbadala kwa nafasi hizo ambazo madaktari hawakuripoti?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kumekuwa na changamoto ya wananchi kulazimika kuajiri walinzi kwa ajili ya kulinda shule za sekondari na zahanati, je, nini mkakati wa Serikali kuajiri walinzi hawa ili waweze kulipwa na mafao yao ya uzeeni? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Kamonga, kwamba kwa utaratibu wa ajira ulioanza mwaka wa fedha 2021/2022. Kwanza ajira zinaombwa kwa njia ya mtandao kwa maana kwa njia ya kielektroniki. Kuna mfumo mahususi wa ajira lakini wanaoomba ajira wanaomba kituo mahsusi kwa maana ya ndani ya halmashauri husika na kituo husika.

Mheshimiwa Spika, tumeshaweka utaratibu kwamba, lazima waripoti na hawawezi kuhamishwa ndani ya miaka mitatu ya

kwanza katika maeneo yao. Naomba kuchukua suala hili la Ludewa, tulifanyie ufuatiliaji kama kuna madaktari walipangiwa na kabla hawajaripoti walihamishwa, tuone ni kwa sababu gani hatua hizo zilichukuliwa kinyume na taratibu za ajira ambazo zimewekwa kwenye mfumo wa ajira kukaa angalau miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuhakikisha kwamba halmashauri zote za pembezoni, zinapangiwa watumishi zaidi kuliko za mijini kwa sababu za pembezoni zina upungufu mkubwa. Tutahakikisha kwamba hatuhamishi bila sababu za msingi kwa watumishi kutoka halmashauri za pembezoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kuajiri walinzi katika shule na maeneo mengine kama zahanati. Tulielekeza kwamba Serikali za Vijiji ziweke utaratibu rafiki kwa wananchi kuona uwezekano wa kulinda rasilimali za shule. Lakini zahanati na vituo vingine vya huduma bila kuwaumiza wale walinzi kwa maana kuwalipa posho zao na kuhakikisha kwamba wanawekewa fedha kwa ajili ya kiinua mgongo pale wanapostaafu kwa taratibu zile za ajira za mikataba, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii. Jimbo la Newala Vijijini lina jumla ya walimu 475 kati ya walimu 787 wanaohitajika kuwepo.

Je, ni lini Serikali itapeleka walimu 312 ambao ni upungufu katika Jimbo la Newala Vijijini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa Kada ya Elimu na pia imeendelea kupeleka walimu katika Halmashairi ya Newala Vijijini lakini tunatambua kwamba bado kuna upungufu. Nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge, kwamba kadri Serikali itakavyokuwa inaajiri walimu, tutatoa kipaumbele katika Halmashauri ya Newala Vijijini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ina upungufu wa watumishi wa Sekta ya Afya takribani asilimia 60 ya mahitaji yake.

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi kubwa sana ya kuajiri wataalam wa afya imefanyika. Jumla ya watumishi wa kada mbalimbali za afya wapatao 17,000 wameajiriwa na kupelekwa katika halmashauri zote kote nchini ikiwepo Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu bado kuna upungufu, namuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba kadri tutakavyoendelea na ajira nyingine za wataalam wa afya, tutatoa kipaumbele kwa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ina upungufu wa watumishi wa kada ya ualimu wapatao 1000 na kada ya afya wapatao zaidi ya 200.

Je, ni lini Serikali itaenda kutatua kero ya watumishi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, utatuzi wa changamoto ya upungufu wa wataalam wa sekta ya elimu na afya ni mchakato, safari ni hatua, tumeanza. Katika Halmashauri ya Tanganyika nafahamu ni moja ya halmashauri ambazo zilipata watumishi wengi sana katika ajira mbili zilizopita ukilinganisha na halmashauri nyingine kwa sababu ya vigezo vya kuwa ipo mbali zaidi lakini ilikuwa na upungufu mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba zoezi ambalo limeanza la kupeleka watumishi kwa wingi Tanganyika, litaendelea kadri tutakavyokuwa tunaendelea kuajiri watumishi wa sekta hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa walimu katika shule za msingi na sekondari Mkoa wa Simiyu hasa walimu wa sayansi; je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa 11 ambayo Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliiainisha ikiwa ni mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi wa sekta ya elimu, lakini pia wa sekta ya afya. Kila ajira zinapotokea, mikoa hii inapewa kipaumbele cha hali ya juu zaidi kuliko mikoa mingine ambayo ina nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo ajira mbili zilizopita walivyopata watumishi wengi Mkoa wa Simiyu, tutaendelea kupeleka watumishi wengi ili waweze kupunguza pengo la watumishi katika vituo lakini na shule zetu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 124

**Kuongeza posho za Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza posho za Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura ya 290, kila halmashauri inatakiwa kuweka utaratibu wa kuwalipa posho, Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za mapato kwenye halmashauri nyingi nchini, Serikali ilianza kutenga bajeti

katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa vijiji.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 22.5 kwa ajili ya kulipa posho za Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa vijiji katika halmashauri 168.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kubuni na kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ya kukusanya na kutumia fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na matumizi mengineyo ili kuongeza uwezo wa malipo kwa viongozi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina mwaka wa nane hapa Bungeni, sijawahi kuona mjadala wowote wa kupandisha posho za Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Napenda Mheshimiwa Waziri atueleze, ni lini mara ya mwisho Serikali ilipitia…

**SPIKA:** Mheshimiwa, hujawahi kuona nini? Samahani.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, sijawahi kuona mpango wa Serikali kupandisha posho za viongozi hawa. Napenda kujua, ni lini mara ya mwisho Serikali ilipitia posho za Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali kwa kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Mama Samia amepeleka fedha nyingi sana vijijini na zinahitaji umakini wa usimamizi ili miradi iweze kukamilishwa kiukamilifu.

Je, kwa mwaka wa fedha ujao 2024/2025 Serikali ipo tayari kuongeza posho ya Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ili kupunguza kelele za viongozi hawa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza namuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika Bunge la Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mjadala ambao Waheshimiwa Wabunge waliujadili kwa kina sana, ilikuwa ni uwezekano wa kuongeza posho za Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti, na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili limeshajadili sana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulipokea, nimhakikishie kwamb lini posho hizi zilipandishwa, posho za Waheshimiwa Madiwani zilipandishwa. Nitakwenda kuona *exactly* ni lini lakini nafahamu kwamba zilipandishwa kutoka zilipokuwa, kidogo lakini sasa angalau ziko na hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba zinahitajika kuongezeka zaidi ili ziweze kukidhi mahitaji na safari ni hatua. Serikali inaendelea kulitazama na kuona uwezekano huo wa kupandisha posho za Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, pili, katika mwaka ujao wa fedha, kama tutaongeza posho hizo au vinginevyo. Tumelichukua, Serikali itafanya tathmini na kuona uwezekano huo na itatoa taarifa rasmi kama linawezekana ama tunahitaji kuijengea uwezo ili kuweza kuongeza posho hizo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa uzoefu ambao nimeupata kujifunza kwenye halmashauri mbalimbali

nchini, kumekuwa na halmashauri nyingi ambazo zinavuka na bakaa kwa maana ya salio.

Je, Serikali haioni ni wakati sahihi kuzielekeza halmashauri zote nchini kutumia mapato ya ndani kuwaongeza Madiwani kwa sababu sehemu kubwa Serikali imechukua mzigo huo na halmashauri nyingi zimekuwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali ni moja.

**MHE. FESTO R. SANGA:** ...zikivuka na bakaa na salio?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kuna baadhi ya halmashauri zimekuwa zikivuka na fedha katika mwaka wa fedha unapoisha kwenda mwaka mwingine kwa maana ya bakaa na Mheshimiwa Mbunge anapendekeza kwamba salio lile litumike kwa ajili ya kuwalipa nyongeza posho Waheshimiwa Madiwani, lakini niseme zile fedha ambazo zinavuka mwisho wa mwaka wa fedha mara nyingi ni fedha za miradi ambayo inasubiri kutekelezwa. Kwa hiyo, ni fedha ambazo tayari ziko *committed,* lakini zinakwenda kutekeleza miradi ile katika *first quarter* ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ni kwamba tunajua kuna umuhimu wa kuongeza posho Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni jambo ambalo tutaendelea kulifanyia kazi na kadri uwezo wa Serikali utakapoongezeka suala hilo litaendelea kushughulikiwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ningependa kufahamu je, Serikali ipo tayari kupitia upya posho kwa ajili ya vikao vya Madiwani kwa kuzingatia umbali wanakotoka kwa

sababu kama Wilayani Muleba tunazo Kata tano Boziba, Kerebe, Rubale, Ikuza na Mazinga ambazo ni za visiwani lakini Waheshimiwa Madiwani wakienda kwenye vikao wanalipwa posho sawa na wale ambao wanatoka pale pale mjini wakati wao wakienda kwenye vikao inawalazimu walale kutokana na umbali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatoa mwongozo wa posho za kujikimu kwa Waheshimiwa Madiwani wanapohuduhuria vikao vya mabaraza na mwongozo ule ulizingatia wale ambao wanatoka mbali wanahitaji kulala, *rate* zao zilikuwa ziko tofauti na wale ambao wanatoka eneo la jirani hawahitaji kulala *rate* zao ziko tofauti.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Halmashauri zote kuzingatia mwongozo ambao uko *very clear* na unaelekeza wanaotoka mbali wanatakiwa kulipwa kiasi gani na wale wanaotoka jirani wanatakiwa kulipwa kiasi gani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, kwa kuwa Serikali imeondoa mzigo ule wa kulipa posho za Madiwani kutoka kwenye Halmashauri na Serikali Kuu sasa ndio inayolipa hizo posho; je, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iko tayari sasa kuelekeza kwamba zile posho zilizokuwa zinalipwa kwa Madiwani sasa zielekezwe kuwalipa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 alichukua jukumu la Serikali Kuu kulipa posho za Halmashauri 168 kote nchini na kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba halmashauri hizi siku za nyuma zilikuwa zinalipa posho za Madiwani, lakini zile fedha zimeendelea pia kupelekwa kwenye maeneo ya miradi mbalimbali. Naomba tuchukue wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba tuone kama zinaweza zikapelekwa kwenye malipo ya Serikali za Vijiji na Mitaa, tutafanya tathmini tuone kama inaweza kutekelezwa ama vinginevyo na tutaleta taarifa rasmi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphance Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ukiukwaji wa kikanuni na hasa kuhusiana na suala zima la ziara ya Kamati za Kudumu za Madiwani na kwamba kila robo ya mwaka Kamati za Kudumu zinatakiwa kutembelea na kuona miradi iliyotekelezwa katika kipindi hicho, ili kuona kwamba fedha zinazotumwa na Serikali chini ya Mama Samia Suluhu Hassan zinasimamiwa na kuona ile *value for money*. Sasa *Finance Committee* peke yake imekuwa ikienda kwenye ziara hii kinyume na kanuni na Kamati nyingine za kudumu zisiende…

**SPIKA:** Swali lako.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nini tamko la Serikali kuhusiana na changamoto hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ziara za

Kamati za Kudumu za Waheshimiwa Madiwani katika Baraza la Madiwani zimewekwa kwa mujibu wa mwongozo ambao umeelekeza Kamati ya Fedha kutembelea miradi, lakini pia Kamati za Kudumu nyingine kama Huduma za Elimu, Afya na Maji na nyingine kutembelea miradi pia kuona utekelezaji wa miradi ile.

Kwa hiyo, nitumie fursa hii pia kuwasisitiza Wakurugenzi na Mabaraza kuzingatia Mwongozo wa Serikali ambao umetolewa ili kuweza kuwa na ufatiliaji wa karibu wa thamani ya fedha katika miradi ambayo inatekelezwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tena maswali moja kwa moja halafu shukrani zenu zote nimeshazipokea, ili tupunguze matumizi ya muda, shukrani zenu zote nimeshazipokea, kwa hiyo, huna haja ya kunishukuru, nenda moja kwa moja na pia Mawaziri vivyo hivyo usianze kumtaja Mbunge nikishamtaja mimi hapa mbele tayari kashatajwa na *Hansard* zinakuwa zimeshachukua jina lake.

Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 125

**Malipo ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ama umehama? Bado uko Viwanda na Biashara unajibu kwa niaba sio?

Haya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madai ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliidhinishwa na kulipwa kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 39 wa mwaka 2006. Serikali iliamua kuwalipa wastaafu hao kwa kuzingatia Sheria za Pensheni za Jumuiya hiyo, sheria na taratibu za fedha, maridhiano ya mwaka 1984 na Sheria Na. 2 ya mwaka 1987, pamoja na Hati ya Makubaliano ya Septemba, 2005 na Hukumu ya Mahakama Kuu ya tarehe 21 Septemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia miongozo tajwa hapo juu Serikali iliandaa utaratibu wa kuwalipa wastaafu na mirathi kwa waliofariki wapatao 31,831 kwa mujibu wa Hati za Makubaliano. Zoezi hilo lilifanyika kwa kipindi cha miaka minane kuanzia Julai, 2006 hadi Novemba, 2013 lilipofungwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kulipa pensheni za kila mwezi kwa wastaafu ambao hawakuwa kwenye mpango wa kuchangia ambao walirejeshwa na kusajiliwa katika daftari la malipo ya pensheni ya kila mwezi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 hadi kufikia Septemba, 2023 Serikali imeshalipa shilingi 1,075,289,494.12 kwa wastaafu 1,744.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulipa pensheni kwa wastaafu wanaostahili kulingana na sheria, kanuni na taratibu za malipo ya Serikali na si vinginevyo, nakushuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali kidogo yana changamoto kwa wastaafu hawa wa Afrika Mashariki, kwa sababu wastaafu hawa wamefungua kesi na ni imani yangu kwamba Serikali inafahamu kesi ya wastaafu hawa.

Je, Serikali iko tayari kuwaeleza wastaafu hawa kwamba malipo yao yalishalipwa na waache kushughulikia kesi yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wazee hawa wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu kufuatilia malipo haya lakini Serikali inasema imewalipa mpaka mwaka 2016 madeni haya yameshalipwa. Sasa Serikali hawa wazee wanadai kitu gani mpaka wamekuwa wakihangaika mpaka kufungua kesi mbalimbali katika mahakama tofauti ili wapate stahiki zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni kweli kama alivyosema wastaafu hawa ambao kwa kweli kimsingi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi walishalipwa na imekuwa ni *tendency* au kawaida kila kunapokuwa na Serikali mpya au *regime* mpya wanafungua madai katika mahakama yetu kudai malipo, lakini kimsingi Serikali tumeshasema na tunaelekeza tena kwamba kwa kweli waelewe kwamba walishalipwa na hakuna kingine zaidi kwa sababu tayari tulishamaliza kama nilivyosema. Kwa hiyo, wasiendelee tena na madai ambayo kimsingi hayana ukweli.

Mheshimiwa Spika, wastaafu hawa hawadai chochote kama nilivyosema walishalipwa kila kitu na tunachoendelea kulipa sasa ni pensheni kwa wale wachache ambao wanastahili kulipwa pensheni, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi nilikuona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ni kuweka tu msisitizo

kwamba wananchi wetu wana haki ya kwenda mahakamani wanapoona wanaweza wakapata haki zaidi, lakini kwa maana ya Serikali ilishahitimisha mchakato huu kwa barua na waliandikiwa barua ya tarehe 31 Desemba, 2013 ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha wanayo, lakini hiyo haizuii wananchi kuwa na haki ya kwenda mahakamani. Kwa hiyo, Serikali haiwezi kuzuia wananchi kwenda mahakamani, lakini kwa maana ya mchakato ulishafanyika, ukahitimishwa kwa barua na iliandikwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante; je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia na kuharakisha malipo ya waliokuwa wafanyakazi wa mashamba ya maua ya P Floral ili kupisha mwekezaji mpya? Ahsante sana.

**SPIKA:** Eeh, sasa nawaza Mheshimiwa Zaytun liko mahususi sana hilo, sina hakika sana kama Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa na taarifa nalo.

Unazo taarifa zake Mheshimiwa ama nikupe nafasi utaonana na Mheshimiwa Mbunge?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nitamwona Mheshimiwa Zaytun Swai pia kama itakuwa kuna ulazima basi alete swali la msingi.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isiweke mfumo kwa wastaafu na ukajulikana kabisa kulikoni kusumbuliwa kuleta barua kila wakati wanapodai madai yao?

**SPIKA:** Hilo ni la Ofisi ya Waziri Mkuu sijui kama limesikika kwa wanaohusika, Mheshimiwa Patrobass Katambi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imekwishakuweka utaratibu kupitia mifuko ya pensheni. Sasa hivi hakuna hitaji la kwamba apeleke taarifa zake, tayari tumeshaweka utaratibu ambao moja kwa moja mtumishi anapoelekea kwenye kustaafu miezi sita kabla taarifa zake zinaanza kuandaliwa na sasa tunatoa pensheni yake ndani ya siku 60 na kama hakuna dosari yoyote hata siku tatu anapata mafao yake. Kwa hiyo, changamoto hiyo tumekwishaitatua.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji hii taarifa kuhusu hawa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya wakati huo wako nchi nzima na Wabunge hawa sijui kwao, pengine hawapo, wako kila mahali hata kwangu wapo na haya madai kama ni kweli hawana nafikiri kuna namna ambayo taarifa haijawafikia kwa uhalisia kwamba hamna chochote. Kwa nini, ni kwa sababu sawa ni haki yao kwenda mahakamani, lakini kama walishalipwa na kila kitu tayari nafikiri ni vizuri wakawa na hiyo taarifa ili anapoenda ajue anapoteza nauli ya kwake mwenyewe kuliko kupoteza nauli kufatilia kitu ambacho hakipo.

Kwa hiyo, sijui mtatumia namna gani pengine hizo barua hazikuwafikia mfanye utaratibu ziwafikie pengine kwa kushirikiana na TAMISEMI mshushe kule mikoani, wilayani hizo taarifa ziwapate wale watu, kwa sababu kwa kweli wanazunguka sana kutafuta hizo haki sasa kumbe hazipo, ni vizuri hiyo taarifa ikaenda vizuri ili wasiendelee na hayo mahangaiko.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 126

**Mapitio ya bei ya nauli za Shirika la Ndege Tanzania**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya bei ya nauli za Shirika la Ndege Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida nauli za safari za ndege hupangwa na soko kulingana na aina ya huduma inayotolewa. *ATCL* kama ilivyo kwa mashirika mengine ya ndege yanayotoa huduma zake kibiashara, nauli zake zinapangwa na soko kwa kuzingatia matakwa ya sheria za ushindani ambapo vigezo vinavyotumika katika kupanga nauli hizo ni pamoja na gharama za uendeshaji ili kuhakikisha kuwa mashirika ya ndege yanahimili ushindani wa soko na kujiendesha kwa tija na ufanisi.

**SPIKA :** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA :** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu mazuri ila nina maswali mawili.

Je, ni kwa nini Serikali haifanyi utafiti wa suala la bei wa safari za ndege za ndani ya nchi kutokana na bei hizo kuwa kubwa sana, kwa mfano Dodoma - Dar es Salaam 200,000 na zaidi mpaka 500,000 kwa safari ya mara moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni hatari ya kupoteza soko la ndani endapo yakajitokeza mashirika mengine yakafanya biashara hii kwa mfano *Flight-Link* inafanya safari hiyo kwa dola 180 sawa na shilingi 450,000 kwa safari ya kwenda na kurudi Dodoma - Dar es Salaam na ni *fixed*. Kwa nini hamuoni mfanye bidii ili kuliokoa Shirika la Ndege Tanzania lisije likazama? Kwa nini hamjiongezi? *(Makofi)*

**SPIKA :** Mheshimiwa Mbunge, mbona umelichagua shirika moja tu kulitaja hapo, ama huwa wanakupa *offer* labda? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma kama alivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, moja kuhusu tafiti, Shirika letu kwanza, mashirika ya ndege sio moja yako mengi kama alivyosema Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa amegusia kwenye *ATCL specific,* ni kwamba tafiti zinafanyika lakini kwa kuwa jukumu la Bunge ni kushauri Serikali tutaongeza pengine utafiti zaidi ili kwenda sambamba na hoja yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja namba mbili ya kwamba je, hatuoni hatari ya kupoteza soko, nadhani ni jambo ambalo pia linazungumzika kupitia utafiti huo ambao tunaenda nao ambao ameusema kama alivyoshauri tutaendelea kujipima, lakini kwa sasa hivi *ATCL* haijapoteza soko kwa sababu ipo kwenye ushindani na viwango vilivyowekwa ni kwa mujibu wa ushindani kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. *(Makofi)*

**SPIKA :** Mheshimiwa Priscus Tarimo swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunapata ndege za moja kwa moja kutoka Dodoma kwenda Kilimanjaro na Arusha au muda mfupi wa kuunganisha kwa kupitia Dar es Salaam?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Priscus Tarimo kuhusiana na kuanzisha *route* inayokwenda Kilimanjaro, nafikiri Serikali itakapokuwa tayari basi ataweza kuarifiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

Na. 127

**Hitaji la mabweni Chuo cha Usafirishaji *(NIT)* Mabibo**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa madarasa na mabweni ya Chuo cha Usafirishaji *(NIT)* Mabibo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali kupitia *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP),* mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, imeanza ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500. Ujenzi wa mabweni hayo umefikia asilimia 28. Aidha, kupitia mradi huo Serikali inajenga jengo lenye Madarasa ya wanafunzi 1,500 pamoja na maabara na karakana yenye kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo (maktaba) chenye madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,653 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi huo kwa sasa upo kwenye asilimia 85.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Chuo, itaanza ujenzi wa Jengo la Kitaaluma la ghorofa tano litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,700 kwa siku, mara litakapokamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, swali la nyongeza.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Serikali nashukuru kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa chuo hichi cha usafirishaji kuongeza wanafunzi wa kigeni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usafirishaji ambacho kiko pale Dar es Salaam kina wanafunzi 14,464 na katika wanafunzi hao asilimia 99.2 ni wanafunzi wa Kitanzania na asilimia 0.8 ni wanafunzi wa nje.

Mheshimiwa Spika, chuo kimeendelea na programu mbalimbali za kuhakikisha kinaongeza wanafunzi wengi kama ambavyo imeulizwa na Mheshimiwa Mbunge ikiwa ni kwa ajili ya kuhakikisha tunaongeza *forex,* lakini pia kwa ajili ya kuongeza *experience* kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, programu mbalimbali zimefanyika katika chuo hicho ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Balozi zetu za nje

kukitangaza chuo chetu kimataifa. Vile vile tumeshiriki katika mikutano mbalimbali mingine imefanyika Nchini Rwanda kwa ajili ya kuongeza na kutangaza chuo chetu.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, chuo chetu kwa sasa kinaandaa mkutano mkubwa tarehe 18 mpaka tarehe 20 mwezi ujao ambao ni *First International Conference on Transport and Logistics and Management* ili kuleta wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuhakikisha kwamba pengine tunaweza kujitangaza zaidi na kupata wanafunzi wengi zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na.128

**Kuunganisha Kodi ya Mapato ya Madini na Mfumo wa *MMMIS***

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, kwa kodi ya mapato kwa wachimbaji wadogo wa madini isiunganishwe na *Mineral Market Management Information System (MMMIS)*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze sana Taifa *Stars* jana kwa kutuandikia historia kubwa sana. Kiongozi akiwa na baraka malango yote yanafanyika, kila linalofanyika kwa sababu ya baraka za Mama Samia linakubali tu ndiyo maana hata Yanga tukaingia makundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuzitaka taasisi za umma kuhakikisha mifumo yote ya mapato na matumizi inasomana, Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuunganisha na kufungamanisha mifumo yake ya usimamizi wa mapato na mifumo ya taasisi nyingine ikiwemo mifumo ya *Mineral Market Management Information System*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Tume ya Madini zimeingia makubaliano ya kubadilishana taarifa ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Aidha, kodi ya mapato kwa wachimbaji wadogo wa madini inakusanywa katika masoko ya madini chini ya usimamizi wa Tume ya madini kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mkoa wa Iringa una *potential* kubwa ya madini ya chuma pamoja na madini ya viwandani, je, Wizara ya Fedha iko tayari kutuunganisha na wadau ili tuweze kutumia *potential* hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mkoa wa Iringa pia umekuwa ukikusanya maduhuli kila mwaka takribani bilioni moja kutokana na madini. Sasa Wizara ya Fedha ipo tayari kuwa na mpango mahususi kuisaidia *GST* na *STAMICO* kufanya utafiti wa kijiolojia ili tuongeze mapato hayo na yenyewe inufaike? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, Wizara ya Fedha tuko tayari na Mheshimiwa Mbunge kabla ya kurudi Jimboni tufanye kikao ili tuweze kumuunganisha na Idara inayosimamia hiyo ili aweze kuwaunganisha na wadau aliowataja kwa ajili ya kufanikisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lile la pili, *GST* pamoja na taasisi zingine kuhusu kuongeza utafiti zaidi, tulishaongea na Wizara ya Kisekta na tuko tayari kuongeza fedha ili utafiti zaidi uweze kufanyika, kwa sababu *potential* ya kugundua maeneo mengine ya uchimbaji bado ipo na inaweza ikatuletea tija zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

Na.129

**Mpango wa kunusuru uchumi wa nchi**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO K.n.y. MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali katika kunusuru uchumi wa nchi kutokana na ukosefu wa fedha za kigeni, hususani Dola ya Kimarekani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi, wa kati na za muda mrefu katika

kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni, hususani dola ya Kimarekani hapa nchini. Changamoto hiyo imesababishwa na athari za mgogoro wa vita kati ya Ukraine na Urusi; kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii baada ya UVIKO-19; na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni utekelezaji wa sera za fedha ambayo inalenga kupunguza ukwasi katika uchumi wa nchi mbalimbali ikiwemo Marekani katika kukabiliana na masuala ya mfumuko wa bei. Kwa ujumla matukio hayo yameathiri mnyororo wa uzalishaji, usambazaji na uhitaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kupunguza athari na changamoto za upatikanaji wa fedha za kigeni ni pamoja na:-

(a) Kuongeza kiwango cha kuuza fedha za kigeni katika soko la fedha za kigeni, ambapo kati ya Machi, 2022 na Agosti, 2023 Benki Kuu ya Tanzania imeuza katika soko la fedha za kigeni zaidi ya dola za Kimarekani milioni 500;

(b) Kuongeza vyanzo vya upatikanaji wa fedha za kigeni ikiwemo ununuzi wa dhahabu;

(c) Kutekeleza mikakati ya kuongeza mauzo ya nchi za nje na kuzalisha bidhaa mbadala wa zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi; na

(d) Kuendelea kushirikisha benki za biashara, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, pamoja na wadau wengine katika kuimarisha sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa fedha za kigeni hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizojitokeza, hali ya upatikanaji wa fedha za kigeni nchini imeendelea kuwa himilivu ambapo akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni

5,246.7 mwezi Julai 2023, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa takriban miezi 4.7 ikilinganishwa na malengo ya miezi minne.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa kuna Wakandarasi wengi wamesaini mikataba na Serikali hasa mikataba ya ujenzi; na kwa kuwa Mikataba hiyo imeathiriwa sana na mabadiliko makubwa ya viwango vya kubadilisha fedha za kigeni hasa dola za Kimarekani. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Wakandarasi hawa ili wasishindwe kutekeleza miradi hiyo hasa miradi ya ujenzi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa mabadiliko ya viwango vya kubadilishia fedha za kigeni kabla hatujapitisha bajeti ya nchi ilikuwa shilingi 2,350, hiyo ni dola ya Kimarekani na sasa ni shilingi 2,500 hadi shilingi 2,600 na mabadiliko haya yameathiri bajeti ya nchi tuliyoipitisha hapa Bungeni hasa kwenye maeneo ambapo Serikali inahitaji kununua bidhaa nje ya nchi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuinusuru bajeti yetu tuliyoipitisha hapa Bungeni ili iweze kutekelezeka vizuri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mazuri aliyouliza Mheshimiwa Ndaisaba; kuhusu swali la kwanza ambalo linahusisha Wakandarasi ambao watakuwa wameathirika na mabadiliko ya bei za kubadilishia fedha huku Mikataba yao ikiwa imeshasainiwa, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na niwaombe Wakandarasi wa aina hiyo kufanya *engagement,* kufanya

mashauriano na sekta zinazohusika kwa sababu masuala ya kimkataba ni ya sekta kwa sekta ili jambo hili liweze kusogelewa kwa umahususi wake katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, tunazo taarifa katika baadhi ya miradi ambako tayari walishafanya mashauriano ya aina hiyo kutokana na mabadiliko haya ambayo yalikuwa yanajitokeza ya kiuchumi. Kwa hiyo hata hawa ambao watakuwa wamekumbwa na jambo hilo, ni vizuri kufanya majadiliano katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jambo la pili la kunusuru bajeti, Serikali inachukua hatua ambapo mpaka hivi sasa tumefanya utaratibu wa kuona namna ambavyo tunaweza tukabana matumizi ya ndani ya Serikali hasa katika maeneo ya matumizi ya kawaida ili kuweza kutoa fursa miradi ya wananchi isiathirike. Hilo ndiyo lilikuwa agizo la Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba, tunafanya utaratibu wa kuangalia matumizi ambayo siyo ya lazima ili fedha ambayo inapatikana iweze kutekeleza miradi ya maendeleo ili bajeti ya miradi ya maendeleo isiathirike.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameendelea kutuongoza katika baadhi ya maeneo kuweza kuhakikisha kwamba tunapata fedha nyingi za kigeni ili ziweze kupunguza tatizo la uhaba wa dola ndani ya nchi na kuruhusu uhimilivu ama ustahimilivu, uimara wa bei ya kubadilishia fedha na uimara wa shilingi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na.130

**Tatizo la mawasiliano ya simu Arumeru Magharibi**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, lini huduma ya Mawasiliano ya Simu itapelekwa Kata za Bwawani, Oldonyowas, Laroi, Mwandet, Oljoro na Oldonyosambu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Noah Saputu, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itafanya tathmini ili kubaini changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata za Bwawani, Oldonyowas, Laroi, Mwandet, Oljoro na Oldonyosambu zilizopo Jimbo la Arumeru Magharibi, tathmini hii itasaidia kufahamu ukubwa wa tatizo na mahitaji halisi ili hatimaye yaweze kuingizwa katika orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha na kutangazwa katika zabuni zijazo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, swalil a kwanza; kwa kuwa wananchi katika karne hii ya leo wanateseka kupanda juu ya vichuguu na vilima kutafuta mawasiliano; je, tathimini hii itafanyika ili wananchi hawa wapate huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliwapa Wizara hii minara mia saba na hamsini na nane.

Je, sasa Wizara haioni ni wakati muafaka Kata za Oldonyowas, Oldonyosambu, Mwandet, Laroi, Oljoro na Bwawani kupata mgao wa minara hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba Watanzania hawapandi kwenye miti, hawapandi kwenye vichuguu ili kupata huduma ya mawasiliano na ndiyo maana Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inajitahidi sana kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba inatatua changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili cha swali la Mheshimiwa Mbunge, ili kufikia kwenye miradi kutangazwa na zabuni kupatikana hatua ya kwanza tunaanza na kufanya tathmini ili kujiridhisha tatizo likoje, tunafanya *feasibility study,* baada ya hapo tunafanya *detailed design* na baada ya hapo tunakuja kutangaza *tender,* sasa hatua ambayo imefikiwa ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiongelea ni hatua ya kusaini Mkataba ambapo tayari pesa zimeshaelekezwa katika maeneo maalum.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo moja kwamba, Serikali tayari imeshapata fedha kwa ajili ya kufanya tathmini katika maeneo yake na tukishakamilisha na fedha zikapatikana, basi tutatangaza *tender* kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasilino kwa ajili ya wananchi wa Arumeru Magharibi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano katika Kata ya Sirop, Wilaya ya Hanang?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kata ya Sirop ina changamoto ya mawasiliano. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki cha Bunge tukutane ili nimuunganishe na watalam wetu ili waweze kumpa tarehe ya kufika katika eneo hilo kwa ajili ya kufanya tathmini, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini Serikali itapeleka minara katika Kijiji cha Misyaje, Kata ya Malumba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kabisa nipokee changamoto hii ya mawasiliano kutoka kwenye hiyo kata, lakini nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa sababu sina taarifa za kina kuhusu kata hiyo ili tuweze kuitazama na kwenda kuchukua hatua stahiki, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwezi, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali; katika Jimbo la Kaliua kuna Kata ambazo ziko kwenye programu ya kupata mawasiliano ya simu hususani Iyagala, Isawima pamoja na Ugunga; je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa kuweka minara katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ujenzi wa minara katika maeneo mbalimbali nchini unaendelea na uko katika hatua mbalimbali. Nimhakikishie kabisa Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumetoa maelekezo kwa watoa huduma, ndani ya Mkataba ambao tumekubaliana nao, hatutowaacha ifike miezi ishirini ndiyo tuseme kwamba umekamilisha au haujakamilisha. Tumepeana kwamba kila baada ya muda fulani watupatie taarifa ya utekelezaji wamefikia wapi ili tuweze ku-*monitor* na ku-*evaluate* kadri mradi wa utekelezaji unavyoenda. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuhusu Jimbo la Kaliua utekelezaji utaendelea na sisi Serikali tunalitazama kwa makini sana ili wananchi wa Kaliua waendelee kupata huduma ya mawasiliano, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Changamoto za mawasiliano zilizopo Arumeru Magharibi zinafanana sana na hali ilivyo kule kwetu Mashariki.

Je, ni lini Serikali itaondoa kabisa changamoto za mawasiliano katika Kata za pembezoni Ngarenanyuki, Leguruki, Maruvango, King'ori na Malula? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ni swali la nyongeza hilo, kwa hiyo sasa ukimjazia yote hayo Mheshimiwa Naibu Waziri…, Mheshimiwa Naibu Waziri chagua Kata moja kati ya hizo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda Watanzania na kwa sababu inataka Watanzania wote washiriki katika uchumi wao wa kidigitali na ni lazima wawasiliane kwa kutumia mifumo ya TEHAMA na sisi kama Serikali ambao ni wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, najitolea kuhakikisha kwamba nitaenda katika Jimbo la Arumeru Mashariki ili tukajionee changamoto ilivyo na tuchukue hatua na hakuna cha kwamba ni kata moja tu, tutahakikisha maeneo yote ambayo yana changamoto kulingana na upatikanaji wa fedha tutafikisha mawasiliano, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kiteto ilikuwa na vijiji vingi sana, sasa kwa mujibu wa mikataba *indication* ni lini, walikubaliana watamaliza kwa kipindi gani? Kwa sababu kesho nina mkutano wa hadhara na haya maswali yatakuwa mengi sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nikishamtaja Mbunge, wewe nenda kujibu swali lake, huna haja ya kumtaja Mbunge mimi nikishamtaja.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, haya nakushukuru, napenda kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye baadhi ya maswali ni kwamba utekelezaji wa miradi hii ya minara 758 kuna hatua kadhaa ambazo zinafanyika na mkataba wetu ukamilishaji wake utaanzia kwenye miezi tisa. Kuna maeneo ndani ya miezi tisa minara itakuwa imeshakamilika na kuna maeneo katika miezi 10, 11 mpaka mwisho wa mkataba wetu itakuwa ni miezi 20 tutakuwa tumehakikisha kwamba minara imeshasimama katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kikubwa sana ili kuhakikisha kwamba Serikali inaendelea ku-*monitor* utekelezaji, tumehakikisha kwamba tumewapatia utaratibu maalum, kila baada ya miezi mitatu wanatoa taarifa ya utekelezaji walipofikia na mpaka sasa watoa huduma wengi wameshatupatia utekelezaji wao, wengine wameshapata vibali, wengine wameshapata benki *guarantee,* kuna wengine bado hawajapata benki *guarantee*.

Kwa hiyo, watoa huduma mbalimbali wako katika hatua mbalimbali, lakini wako ndani ya muda ambao tumekubaliana. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Watanzania kwamba utekelezaji huu utaenda kama ambavyo umepangwa.

**SPIKA:** Ahsante sana.  Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, Kata ya Kirogo wananchi wa Kata hii ili kufanya mawasiliano wakati mwingine huwalazimu kupanda juu ya milima, na kwa kuwa Kata hii ipo kwenye ile miradi ya kidigitali, ninataka nijue *commitment* ya Serikali, ni lini miradi hii itaanza ya ujenzi wa minara kwenye Kata hii ya Kirogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, mradi huu umeshaanza na upo katika hatua mbalimbali. Tunaamini kwamba Jimbo la Rorya watafika kwa ajili ya utekelezaji huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu Kata ya Mapanda na Kibengu katika Jimbo la Mufindi - Kaskazini kwa sababu wananchi wanapata shida sana ya mawasiliano? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, maeneo ya Kibengu hayapo katika minara 758 lakini tunayaingiza kwenye tathmini ya minara kwenye vijiji 2,116. Kwa hiyo, tukishakamilisha na fedha zikapatikana, tutafikisha mawasiliano katika Kata hiyo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Ilolanguru, Kata ya Ikobe, Kata ya Iponya na Lubembela zinakabiliwa na changamoto ya mawasiliano. Waziri lini utapeleka mawasiliano Wilaya ya Mbogwe katika Kata hizo nilizozitaja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Maganga kuna maeneo ambayo yanafanyiwa tathmini lakini kuna maeneo ambayo yapo ndani ya miradi 758. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge miradi hii itakapokamilika lakini na yale ambayo tumeyaingiza kwenye tathmini na fedha zikapatikana

tutafikisha mawasiliano ndani ya Jimbo la Mbogwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu Jimbo la Ngara, Kata ya Murukulazo kwa sababu mawasiliano yanasuasua? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa eneo hilo lina changamoto kwa sababu liko mpakani kule na linapata huduma kutoka maeneo ya ndani ambapo minara yake haina nguvu sana. Tulishatuma wataalam wetu katika maeneo haya kwa sababu yapo katika miji ambayo ni ya kimkakati na Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba, maeneo yote ya kimkakati tunahakikisha tunaimarisha huduma ya mawasiliano. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane naona umesimama muda mrefu, jana uliuliza swali kwenye eneo hili ama siyo hili?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, hapana sikuuliza jana.

**SPIKA:** Haya sawa, ahsante. Karibu kwa swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza kujenga minara 15 iliyopangwa kujengwa katika Wilaya ya Kilwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, tayari mradi wa Tanzania ya kidigitali

minara 755 kwenda kwenye kata 713, Wilaya 112. Ninakuhakikishia kwamba iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hivyo ninamuomba Mheshimiwa Mbunge tuwe na subira kwa sababu ujenzi wa minara ni hatua, hatua hizo zikishakamilika kusimamisha mnara wenyewe hauchukui hata miezi miwili. Kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kutoa ushirikiano katika maeneo ambapo wataalamu wetu watakapofika kwa ajili ya kupata maeneo na vibali basi awe sehemu ya ufanikishaji huo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake.

Na. 131

**Ujenzi wa barabara ya Njia Panda hadi Lalago kwa kiwango cha lami – Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Njia Panda - Mangola - Matala hadi Lalago kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njia Panda kuanzia Karatu – Mang'ola – Matala –

Sibiti River hadi Lalago, yenye urefu wa kilometa 328 inayojulikana kama *Eyasi Route*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kuanzia *Sibiti River* hadi Lalago yenye urefu wa kilometa 121 imejumuishwa kwenye mradi wa *EPC+F* kupitia barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – *Sibiti River* – Lalago hadi Maswa ambayo ina jumla ya kilomita 389 ambapo mkataba wake wa ujenzi umesainiwa. Kwa sehemu iliyobaki ya Njia Panda – Mang'ola hadi Matala kilometa 137, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii imeahidiwa toka Serikali ya Awamu ya Nne na iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Je, ni lini Serikali sasa itatenga angalau kwa kilomita chache ili kuwezesha wananchi wale wa Bonde la Eyasi kuweza kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko ya nchi ya jirani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tunatambua kwamba barabara hii ni muhimu sana. Kama nilivyosema katika jibu la msingi, barabara hii ilitakiwa ijengwe lakini imejengwa barabara ambayo ni *Serengeti Southern Bypass.*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inachofikiria kufanya ni kujenga walau kilometa 50 ambazo zitaanzia pale Njia Panda hadi eneo la Mang'ola ambalo lina uzalishaji mkubwa sana na hasa zao la vitunguu. Kwa hiyo, Serikali sasa inafikiria kulifanya halafu baadae ndiyo ije kukamilisha kipande kilichobaki ambacho kinapita sehemu kubwa ya mbuga, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, hali ya Daraja la Mto Ubagwe hali ni mbaya sana na Mheshimiwa Waziri ni shahidi alituma watu wa *TANROADS*.

Ni lini Serikali inaanza ujenzi wa daraja hili ili kuwanusuru wananchi na hali ya mvua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu na tumefanya mawasiliano makubwa, nimtoe shaka naamini daraja hilo ambalo ni muhimu sana kwa Wilaya ya Ushetu litaanza kujengwa kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mpanda – Uvinza – Kasulu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, barabara hii tumeshakamilisha usanifu na itakuwa ndiyo barabara kuu ya kutoka Kusini kwa maana ya Mpanda – Uvinza hadi Kasulu ambayo haizidi kilometa 57.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kweli inatafuta fedha ili iweze kukamilisha hicho kipande ambacho ndiyo kimebaki peke yake katika Mkoa wa Kigoma, barabara kuu ambayo haina lami. Kwa hiyo, tunalifahamu na Serikali imeendelea kutafuta fedha ili kukamilisha kipande hicho kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na jibu la swali la msingi, kwamba tayari barabara hii imeshasainiwa mkataba. Naomba kuiuliza Serikali baada ya kusaini mkataba ni muda gani Mkandarasi huyu anaanza kujenga hiyo barabara ya Karatu – Haydom – Maswa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara nyingi ambazo ziko takribani sita, ziko kwenye *EPC+F,* baada ya kusaini nilijibu hapa kwamba, wakandarasi wameendelea kuoneshwa hayo maeneo na barabara hizi zinasimamiwa na makao makuu.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa ikiwepo na hiyo barabara ambayo inapita kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ni kuwaonesha wakandarasi, wakandarasi kuzigawa zile barabara kwenye vipande *(lots)* zaidi ya nne na kutafuta wakandarasi wengine ambao watasimamiwa na huyo mkandarasi mkubwa kwa ajili ya kujenga hizo barabara. Kutakuwa na vipande visivyopungua vinne katika kila barabara, kwa maana ya makambi, kutafuta maeneo ambayo yana *raw materials,* kwa maana ya kokoto na changarawe, tayari wako wanapita na kujitambulisha kwenye hizo barabara. Kwa hiyo, mchakato unaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kutengewa fedha kwenye bajeti, bado hakuna hatua yoyote ambayo imeanza mpaka sasa.

Ni lini Serikali itaanza taratibu za ujenzi wa barabara ya lami ya kutoka Korogwe – Dindila – Soni mpaka Bumbuli? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii anayoitaja Mheshimiwa Mbunge tumeitengea bajeti, kwa maana ya utekelezaji wa mwaka huu wa fedha, tayari *tender documents* zinaendelea kuandaliwa ili barabara hiyo iweze kutangazwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ninaomba kujua Mheshimiwa Naibu Waziri umepita sana barabara ya Sanzati kwenda Nata. Sasa ni lini hiyo barabara itamalizika maana imekuwa kero kwa wananchi wa Bunda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba, Mkandarasi tayari yuko *site* anafanya kazi. Nawahimiza Watendaji wa *TANROADS* pamoja na Meneja wa Mkoa ambao wanamsimamia Mkandarasi, kuhakikisha kwamba wanamsimamia ili aongeze kasi na kukamilisha barabara hiyo ambayo inahitajika sana kwa wananchi wa Bunda pia wananchi wa Wilaya ya Serengeti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona; barabara ya Pachayamindu – Ngapa kuelekea Nachingwea, ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatafuta fedha ili kwanza iweze kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, baada ya hapo

gharama itajulikana na Serikali itafuta fedha kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini kipande cha barabara cha kuanzia Malagarasi – Mpeta mpaka Uvinza kitakamilishwa kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kusimamia utekelezaji, kwa sababu hicho kipande alichokitaja cha kilometa 51.3, Mkandarasi yuko *site*, tukisaidiana na mwenzetu wa Abu Dhabi. Kwa hiyo, ni suala tu la kuwasimamia kuhakikisha kwamba wanakwenda kwa kasi ili kiweze kukamilika, maana ndiyo kipande pekee kilichobaki cha vumbi kutoka hapa hadi Kigoma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, miradi ambayo itaendeshwa na *the so-called EPC+F,* ni programu ambayo ililetwa na Serikali hapa Bungeni, lakini majibu ya Waziri unavyojibu ni kama vile huna uhakika hizi barabara zitakamilika lini. Sasa unataka kutuambia wakati mnaandaa hiyo programu, mlikuwa hamjajua zile barabara mlizolenga changamoto zake zikoje, mahitaji yake yakoje na yatafanikiwa vipi? Maana majibu yako hayaeleweki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuja na mpango huu uko kwenye bajeti na inajua itafanyaje, lakini mpango mpya kabisa katika nchi yetu. Kwa hiyo, kinachofanyika na ndiyo taratibu zake kwamba unakuwa na Mkandarasi mmoja katika kila barabara, mkandarasi mkubwa kwa sababu barabara ni ndefu, anakuwa na *sub-contractors* ambao ni lazima ajiridhishe na afanye

tathmini pia ya kwake kwa sababu, yeye ndiye anayesimamia ujenzi wa zile barabara, kwa maana yote kwamba *EPC (Engineering Procurement)* na yeye ndiyo anayefanya pia *procurement*. Kwa hiyo, lazima baada ya kumkabidhi ile barabara ajiridhishe namna pia atakavyogawa hizo barabara.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Serikali ni kumpa fedha na kazi hizo zinaendelea, walioko kwenye zile barabara sasa hivi wako wanaoneshwa zile barabara. Kwa hiyo, watakapoanza, watakuwa pia wamejiridhisha maana yake baada ya kukubaliana hakutakuwa na *variation* kwenye hizo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza Serikali Bunge lililopita iliahidi kujenga na kusaini barabara ya Bigwa – Kisaki hadi sasa ipo kimya; je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Bigwa – Kisaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, barabara hiyo imeshapata mkandarasi na sasa hivi kinachoandaliwa tu ni taratibu za kuisaini hiyo barabara. Kwa hiyo tuna barabara kama 16 ambazo zinaandaliwa utaratibu mzuri wa kuzisaini ili Wakandarasi waanze kazi, ikiwepo na hiyo barabara ya Bigwa – Kisaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi; barabara ya Bungu kuelekea Kibirizi ambayo inamilikiwa na *TANROADS* hali yake ni mbaya sana na haipitiki kwa sasa. Je, mna mpango gani wa kukarabati barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri barabara hiyo naifahamu sana, siyo barabara ndefu ni barabara ambayo ipo katikati ya Mji. Naomba nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa *TANROADS* aipitie hiyo barabara na iweze kukarabatiwa kwa sababu imetengewa fedha kwenye matengenezo ya kawaida. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge barabara hiyo itakarabatiwa katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Masama Kusini walifanyiwa tathmini kupisha ujenzi wa daraja la Kikafe na muda mrefu wamekuwa wakiahidiwa watalipwa fidia na kuthaminishwa fedha. Sasa wameanza kupata matatizo ya kisaikolojia.

Je, wakati mnapokuja kulipa fidia mtawalipa na fidia ya matatizo ya kisaikolojia? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali lako nafikiri liende kama swali la msingi kwa sababu linahusu fidia, swali la msingi hapa linahusu ujenzi wa barabara. Nafikiri likienda kama swali la msingi atakuletea majibu yale ambayo wananchi wataweza kuridhika zaidi kuliko likija kama swali la nyongeza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale sasa aulize swali lake.

Na. 132

**Kukamilika barabara ya Ulinzi ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, lini barabara ya Ulinzi ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere inayojengwa toka Liwale hadi Mahenge itakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kiulinzi na kijamii na inayounganisha Mikoa ya Lindi na Morogoro, katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi milioni 143.04 zimetengwa kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu wa awali. Kazi ya upembuzi yakinifu wa awali itakapokamilika katika barabara hii inayopita katika Hifadhi ya Mbuga ya Wanyama ya Selous, itaonesha iwapo mradi unakidhi vigezo vya uhifadhi mazingira ili kuwezesha kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri yanayotia tumaini kutoka Serikalini. Vilevile ninashukuru kwenye ile barabara yangu ya Nachingwea – Liwale, tarehe 12 yule mkandarasi anaenda kukagua. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hivyo, nina maswali mawili; barabara hii niliyoitaja inayounganisha Morogoro, tayari *TANAPA* wameshaanza kuichonga. Sasa tunachotaka kujua; je, sisi tunaweza kuanza kupita hata kabla ya huo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliotajwa?

Swali la pili, tayari kwenye bajeti iliyopita tunayo barabara yetu ya Nangurukuru – Liwale kilometa 230. Tulishapewa kilometa 72 wananchi wa Liwale wanataka kujua ujenzi unaanza lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Liwale kwenda Mahenge ambayo inapita katikati ya Hifadhi ya

Mwalimu Nyerere, tumetenga fedha kama nilivyosema. Kwa maana ya kutumika kwa sasa waliofanya hiyo barabara ni wenzetu wa Maliasili na Utalii kwa shughuli zao, lakini sisi kama Wizara tunapokwenda kuifanyia upembuzi yakinifu ni kwa maana ya wananchi waweze kutumia.

Mheshimiwa Spika, tuna hakika kama tutakavyokuwa tumefanya usanifu, wenzetu wa maliasili watashauri ijengwe vipi ili iweze kutumika kama barabara ya kiulinzi, pia, iweze kuwahudumia wananchi wote wa Tanzania bila kujali ni wa hifadhi ama siyo hifadhi, ndiyo maana Serikali imetoa fedha ili kurahisisha mawasiliano kati ya wananchi wa Liwale na Mahenge. Kwa hiyo, itaanza kutumika na wananchi kama itakuwa imekidhi hivyo vigezo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili; ni kwamba, Barabara ya Nangurukuru – Liwale tumetenga tuanze ujenzi mwaka huu kilometa 72 kuanzia Liwale kwenda Nangurukuru. Ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari taratibu za manunuzi za awali zimeanza ili barabara hii ianze kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba sasa aulize swali lake.

Na. 133

**Ujenzi wa kivuko cha juu eneo la Magari Saba Mbezi**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kujenga kivuko cha juu barabara ya njia nane eneo la Magari Saba Mbezi ili kulinda uhai wa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Magari Saba, eneo la Mbezi, limekwishawekwa kivuko cha pundamilia *(zebra crossing)* kwa wapita kwa miguu ili kuwawezesha watumiaji wa barabara hiyo kuvuka kwa usalama katika eneo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kutekeleza miradi yetu kwa haraka sana, lakini pamoja na hilo naomba niulize maswali au maombi mawili kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, moja, hapo ambapo tumewekewa kivuko cha pundamilia na taa sasa hivi tunavuka salama, lakini inatubidi tutembee mita sabini pembezoni mwa barabara ili tuingie kwa Musuguri ambapo jioni tunagongwa sana na magari. Ni ombi kwa Serikali, haioni sababu au haja ya kutengeneza Barabara ya wapita kwa miguu katikati ya *road reserve* ili tuweze kuingia kwa Musuguri kwa usalama?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa chini hapa kwenye makutano ya Magari Saba na Mbezi kuna kivuko kingine ambacho Serikali imeanza kukijenga kwa kuweka taa, lakini imekiacha kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itakamilisha taa zile ili nah apo wananchi wavuke kwa usalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mawili ya nyongeza na pongezi.

Mheshimiwa Spika, hili suala ni la utekelezaji. Naomba nichukue nafasi hii kumuagiza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na *TANROADS* Makao Makuu waende wakaone uwezekano wa haya mawazo ya Mheshimiwa Mbunge kuona namna watakavyofanya ili wananchi waweze kutumia haya maeneo ya *road reserve* ili waweze kupita kwa usalama katika eneo hili. Hili ni suala la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, na suala la pili pia ni utekelezaji kwa sababu, mkandarasi yuko *site,* waweze kumsimamia na kuhakikisha kwamba, anakamilisha kazi ambayo anaendelea nayo ya kukamilisha mataa, ili kuweza kuleta usalama hapa katika hii barabara ya njia nane. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 134

**Kuviendeleza viwanda vya nyama na samaki**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaviendeleza viwanda vya nyama na samaki Mkoani Rukwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exhaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa sekta ya viwanda ikiwemo viwanda vya nyama na samaki katika Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine nchini ni endelevu. Serikali inaendelea na juhudi za kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vipya na uendelezaji wa viwanda vilivyopo katika sekta ya mifugo na uvuvi hususani viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa malighafi ya mazao ya mifugo na uvuvi inayovikabili viwanda vya nyama na samaki katika Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine nchini. Kwa sasa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka nguvu kubwa katika unenepeshaji wa mifugo pamoja na ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba, kutenga na kuboresha maeneo ya ukusanyaji samaki *(collection centers)* pamoja na minada ya mifugo ili kukidhi haja ya upatikanaji endelevu wa malighafi bora ya viwanda vya nyama na samaki nchini ikiwemo katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea na juhudi za kukabiliana na tatizo la utoroshaji wa mazao ya samaki na mifugo kwenda nchi za jirani bila kufuata taratibu ili kukidhi mahitaji ya malighafi katika viwanda vyetu vya ndani. Hivyo, nitoe rai kwa wavuvi na wafugaji kuviuzia malighafi viwanda vyetu vya ndani ili viweze kukidhi mahitaji yake, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Mkoa wa Rukwa ukepakana na maziwa mawili likiwemo Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa. Serikali ina mpango gani wa kuanzisha uvuvi wa vizimba katika maziwa hayo, ili kupata malighafi ya samaki kwa wingi?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili; nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kukiendeleza Kiwanda cha SAAFI kilichopo Mkoa wa Rukwa ambacho kilianzishwa na Hayati Chrisant Mzindakaya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwanza nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua umuhimu wa ufugaji wa samaki kwa njia ya kisasa, kwa maana ya vizimba katika Maziwa ya Rukwa na Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tayari imeshaanza zoezi hilo. Tumeanza katika Mkoa wa Mwanza kwa maana ya Ziwa Victoria, tayari tunafuga kupitia vizimba. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wataalamu wetu waweze kutembelea kwenye maziwa haya kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, ili waweze kuanzisha ufugaji wa samaki kupitia vizimba katika Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika na ninakuomba Mheshimiwa Mbunge uweze pia, kushirkiana nasi ili uweze kuwa kinara katika ufugaji huu wa kisasa wa samaki.

Mheshimiwa Spika, pili; kuhusiana na kiwanda hiki cha *Sumbawanga Agricultural and Animal Food Industries Limited* kwa maana ya SAAFI, changamoto kubwa ilikuwa ni fedha na uendeshaji wa kiwanda hiki ambacho ni kiwanda cha kisasa sana hapa nchini. Serikali tayari imeshaanza kupitia Benki ya Uwekezaji Tanzania *(TIDB),* kutafuta mwekezaji mpya baada ya changamoto zilizokuwepo kwa mwekezaji yule wa mwanzo.

Kwa hiyo, tumeshatangaza tayari kupitia gazeti mwezi wa Agosti, kupata mwekezaji mpya ili aweze kuingia ubia na waliopo ili kuhakikisha kiwanda hiki kinafufuliwa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika kutekeleza Sera ya Tanzania ya Viwanda, nini mkakati wa Serikali kufufua viwanda vilivyopo katika Mkoa wa Kilimanjaro ili kuwapatia wananchi wetu ajira, lakini pia kuongeza uchumi wa Mkoa wetu wa Kilimanjaro? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, sijasikia vizuri kiwanda gani, Mkoa wa Kilimanjaro tunachotakiwa kukichukua?

**NAIBU SPIKA:** Amesema viwanda vyote vilivyoko Mkoa wa Kilimanjaro.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nakushukuru, kama nilivyosema nia ya Serikali ni kuhakikisha tunaendelea kutekeleza sera ya kuwa nchi ya viwanda na kama tulivyosema tuwe na uchumi unaoendeshwa na viwanda hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kutafuta wawekezaji kwa sababu, tunaondokana na uchumi hodhi, kwa maana ya Serikali kufanya biashara au kuendesha viwanda. Kwa hiyo, Mkoa wa Kilimanjaro na Mikoa mingine ambako kuna viwanda vyenye changamoto, vile ambavyo vitakuwa vimebinafsishwa, lakini havijaendelezwa au vingine ambavyo tunaona havifanyi kazi, tutaendelea kutafuta wawekezaji kwa kuweka kwenye masharti nafuu, pia vivutio mbalimbali ili kuvutia uwekezaji wa ndani, hata wawekezaji kutoka nje ili kuhakikisha viwanda hivyo vimefanya kazi na kupunguza nakisi ya bidhaa mbalimbali ambazo zinatumika nchini kuagizwa nje, lakini pia kutoa masoko kwa malighafi ambazo zinatumika kwenye viwanda hivyo ambavyo vinzalishwa hapa nchini, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swali lake.

Na. 135

**Ujenzi wa geti jipya Hifadhi ya Mikumi**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza:-

Je, mchakato wa ujenzi wa geti jipya la kuingilia Hifadhi ya Mikumi kutokea Kilangali na Tindiga umefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Londo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha tathmini ya awali kwa ajili ya kujenga lango la kuingilia watalii kupitia maeneo ya Kilangali na Tindiga Wilaya ya Kilosa. Kufuatia tathmini hiyo, gharama za ujenzi wa lango hilo na miundombinu ambata ya lango husika ni jumla ya shilingi bilioni 2.8. Aidha, michoro pamoja na *BOQ* imekamilika. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa lango hilo. Kwa ujumla, lango husika litafungua fursa za watalii watakaosafiri na treni ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam na Dodoma kuingia Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kwa kuona umuhimu wa hifadhi hiyo imejipanga kuongeza malango ya kuingilia watalii katika maeneo yote muhimu ambapo kwa sasa kupitia Mradi wa Kukuza Utalii Kusini *(REGROW)*, malango mawili ya kisasa yanajengwa kwa ajili ya kuingilia watalii katika maeneo ya Doma na

Kikwaraza (Mji mdogo wa Mikumi). Ujenzi huo umeanza mwezi Agosti, 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, Sera ya Ugatuaji ni Sera ya Kitaifa. Suala la mapato ya taasisi zetu na maduhuli ya Serikali kwenda moja kwa moja hazina inaenda kinyume na hii Sera ya ugatuaji. Ndio inayosababisha miundombinu muhimu kwenye hifadhi zetu kutotengenezwa mara kwa mara. Je, Serikali haioni wakati umefika sasa wa kurudisha walau asilimia 20 ya mapato kwenye hifadhi zetu, ili washughulikie miundombinu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali inakiri kufunguliwa kwa geti hili katika Kata ya Kilangali na Tindiga kunaenda kufungua fursa za kiuchumi. Je, wamewaandaa vipi wananchi wa Kata za Tindiga, Dhombo, Masanze na Kilangali, ili wasije kuwa wageni wakati fursa hizi ambazo zitatokana na kufunguliwa kwa lango hili zitakapowadia? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto ya kukamilika kwa miundombinu kwenye maeneo yetu kutokana na kukosekana kwa fedha na mabadiliko tuliyokuwa tumefanya ya mfumo wa kukusanya mapato na kuyapeleka moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Hata hivyo, baada ya jambo hili kujadiliwa kwa kina ndani ya Bunge lako Tukufu na jambo hili kufikishwa Serikalini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kurejesha tozo ya maendeleo ya utalii ambapo tayari Mheshimiwa Rais ameridhia asilimia tatu ya fedha hizi iweze kutumika kwa ajili ya shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili; jukumu la kutoa elimu kwa wananchi wetu sio jukumu la Serikali Kuu peke yake ni pamoja na halmashauri zetu. Nitoe rai kwa halmashauri husika ziweze kutoa elimu kwa wananchi, tukiwepo sisi Waheshimiwa Wabunge, ili wananchi waweze kuchangamkia fursa za kimaendeleo zinazokuja katika maeneo yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha lango la kuingia Mlima Kilimanjaro la Kidia kwani lango hili litakuwa linatumiwa na watu maarufu kupanda Mlima Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika kuongeza mapato katika nchi yetu. Kwa hiyo, ni makusudio ya Serikali kuboresha malango katika hifadhi zetu zote za Taifa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hili la Kidia, tayari Serikali inaendelea na kuboresha eneo lile. Tayari tunavyozungumza barabara ya kilometa karibu 28 ya watembea kwa miguu kwenye eneo lile imeboreshwa. Barabara karibu kilometa tisa inajengwa kwa kiwango cha changarawe na katika bajeti ya mwaka huu kupitia *TANAPA* zimetengwa karibu milioni mia tisa kwa ajili ya kujenga mageti kwenye eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi sasa aulize swali lake.

Na. 136

**Hitaji la Balozi katika nchi za Iran na Pakistan**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafungua Ofisi za Balozi katika nchi za Iran na Pakistan?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua ya kufanya tathmini ya kuangalia uwezekano wa kufungua ubalozi katika nchi za Iran na Pakistan. Tathmini hiyo inayofanyika, inajumuisha pamoja na mambo mengine, kuangalia fursa za kiuchumi ambazo nchi yetu itanufaika nazo kwa kuzingatia mwongozo wa Sera ya Mambo ya Nje uliojikita katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi na tija katika matumizi ya fedha za Umma. Taarifa ya Tathmini hiyo itawasilishwa kwa mamlaka husika pindi itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Tanzania inawakilishwa nchini Iran na Pakistan kupitia ubalozi wetu ulioko Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, Nchi ya Iran ina miaka 56 ya ubalozi hapa nchini, lakini nchi ya Pakistani ina miaka 40 ya ubalozi hapa nchini.

Je, Serikali haioni muhali kidiplomasia kwa miaka yote hii kutokufungua ubalozi kwenye nchi hizi mbili?

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, swali la pili, kama nilivyosema kwa wingi wa miaka ya balozi hizi ambazo ziko hapa kwetu nchini na Serikali kwa kufanya tathmini kwa miaka 56 na miaka 40. Je, *commitment* yake ni lini sasa itafungua balozi kwenye nchi hizi mbili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na kwamba, nchi yetu haina ofisi za ubalozi nchini Pakistan na Iran, lakini hata hivyo tumekuwa na ushirikiano mkubwa na tumekuwa tukishirikiana katika nyanja mbalimbali. Tuna mikakati mingi ya kuendeleza uhusiano huu na mmojawapo ni kuanzisha tume za pamoja za kudumu za ushirikiano kati ya Tanzania na Pakistan na Tanzania na Iran. Kwa Iran tayari hiyo ipo na kwa Pakistan tayari tumeshaanza mchakato huo na tayari tumewasilisha rasimu ya makubaliano hayo na ipo upande wa Ubalozi wa Pakistan tukisubiri majibu yao.

Mheshimiwa Spika, lingine, nchi yetu inapenda kuwa na balozi nyingi sana nchi za nje, lakini ni muhimu sana kufanya tathmini, kama nilivyoeleza hapo mwanzo, ili kujua tija hasa ambazo tutapata katika nchi hizo. Pia hali ya kifedha inaporuhusu nafungua hizo balozi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya. Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mbunge wa Mtoni sasa aulize swali lake.

Na. 137

**Toto Afya Kadi kwa watoto waliokuwa wakilipiwa na wahisani**

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia upatikanaji wa Bima ya Afya kwa watoto wasio na wazazi ambao walikuwa wakilipiwa bima na wahisani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mbunge wa Mtoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mfumo wa kulipia watoto kupitia Toto Afya Kadi umebadilika na kwa sasa unafanyika kupitia utaratibu wa shule na vifurushi vya bima ya afya vya najali, wekeza na Timiza.

Mheshimiwa Spika, suluhisho la kudumu la tatizo hili, ni kukamilika kwa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao tunaamini utawezesha watoto wengi zaidi wasio na changamoto ya kiafya na wenye changamoto za kiafya kulipiwa Toto Afya Kadi. Hatua hii itasababisha kuwepo kwa uhai na uendelevu wa Mfuko wa Bima ya Afya, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika nashukuru, nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali imeshapeleka elimu kwa Wakuu wa Shule na Kamati za Shule hasa shule za Serikali zilizoko vijijini kwamba ipo huduma hii ya afya kwa watoto na inaweza kupatikana kupitia shule? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, anasema kama Serikali imeshapeleka. Ni kweli tumeshaanza kupeleka na kwa sababu suala la elimu ni endelevu, tunaendelea kupeleka, lakini pia nilitumie Bunge lako tukufu, nawaomba Wabunge kwenye mikutano yetu ya kwenye Wilaya zetu, tuendelee kuwasisitiza wananchi na watu wengine na Serikali ya Wilaya na watu wengine kuhakikisha wanahamasisha hili na kuwapa taarifa wazazi, tufanye hilo kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, Serikali inatumia utaratibu gani kuwapatia matibabu watu wenye ulemavu wasiokuwa na uwezo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa kutoa matibabu bure kwa watu wasio na uwezo wa kujilipia. Kwenye eneo lake la kata yake, akishapata barua ya Katibu Kata akienda hospitali na kuna watu wa Maendeleo ya Jamii kwenye kila hospitali yetu, ambao wanashughulikia mambo hayo na wanaweza kumsaidia na akapata huduma bure kama hana uwezo wa kujilipia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.

Na. 138

**Kukamilisha Vituo vya Polisi Lupa**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi kwa kumalizia ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Itumbi na Kambikatoto, Lupa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Polisi vya Itumbi na Kambikatoto ni vituo vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi na mpaka kumalizika ujenzi wake vitagharimu kiasi cha fedha shilingi 279,780,978. Fedha inayohitajika ili kumalizia ujenzi kwa kuunga mkono nguvu za wananchi, ni shilingi 173,447,178. Fedha hizo zitatoka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ili kumalizia ujenzi huo kama njia ya kuwaunga mkono wananchi wa Jimbo la Lupa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri na tunaona namna ambavyo wanatuunga mkono na sisi tunasema ahsante. Tunaiomba tu Serikali tuweze kupata hizi fedha kwa wakati ili hivi Vituo vya Polisi viweze kukamilika.

Nina maswali mawili madogo ya nyongeza; Kituo cha Polisi cha Chunya Mjini ni Kituo cha Polisi cha zamani toka ukoloni, kidogo na kiko ndani ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya; je, ni upi mpango wa Serikali kuwezesha kujengwa kituo kikubwa cha Polisi chenye hadhi ya wilaya katika Wilaya yetu ya Chunya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wilaya ya Chunya ina changamoto kubwa ya nyumba za askari; je, ni upi mpango wa Serikali kuweza kujenga nyumba za askari ili waondokane kuishi katika mazingira magumu katika Wilaya ya Chunya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Wizara kupitia Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba Wilaya zote nchini zinapata vituo vyenye hadhi ya Wilaya ambavyo vitakuwa na *OCD*, *OC-CID*, askari wa idara nyingine na askari wa kawaida ili kuwezesha ulinzi wa raia na mali zao. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali kulitekeleza hili bado ipo na nikuahidi kwamba katika mpango wake wa miaka 10 ambapo sasa hivi miaka miwili imepita ya ujenzi wa vituo hivi, tutahakikisha kituo cha wilaya yako kinaingia katika mpango angalau mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba tumwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapojenga Kituo cha Polisi cha ngazi ya Wilaya au vituo vya Polisi daraja C ngazi ya kata na tarafa, tuhakikishe eneo linakuwa kubwa la kutosha kwa ajili ya kujenga kituo pia na makazi ya askari na viongozi wao. Kwa hiyo, wilaya ikituhakikishia uwepo wa viwanja hivyo tutaingiza kwenye mpango wa ujenzi wa kituo pamoja na nyumba, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, katika Mji wa Njombe tuna Kituo cha Polisi ambacho hakina hadhi ya makao makuu ya mkoa; je, ni lini kituo

chenye hadhi ya mkoa kitajengwa katika Halmashauri ya Mji wa Njombe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba mikoa yote ambayo haina vituo vya ngazi ya mkoa, vinajengewa vituo hivyo. Tumeanza kwa awamu katika maeneo mengine na Njombe ni eneo lingine ambalo litapewa kipaumbele katika mwaka ujao wa fedha, kuanza kujenga Kituo cha Polisi ngazi ya mkoa, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Gereza la Wilaya ya Nyang'hwale kwa sababu huduma hiyo tunaipata kwa umbali mrefu sana zaidi ya kilometa 100? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, japo swali ni la polisi, lakini nakubali tu kwamba ni nia ya Serikali kadri huduma za magereza zinapokuwa mbali zinaongeza gharama za kusafirisha washtakiwa au mahabusu kutoa eneo lile kwenda enei lingine ambapo bado inakuwa ni sehemu ya gharama za Serikali. Nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu nina ahadi ya kutembelea Jimbo lake la Nyang'hwale tutajiridhisha kuona eneo kama lipo la kutoa ili Jeshi la Magereza liingize katika mpango wake wa ujenzi, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nami niulize swali dogo la nyongeza. Waziri unacheka kwa sababu unajua ninachouliza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Bunda hakina hadhi ya Wilaya na kinahudumia majimbo matatu; ni lini sasa mtatuhakikishia mnatujengea kituo chenye hadhi ya Wilaya na hii ni zaidi ya mara kumi nakuuliza wewe hapo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, swali analoliuliza Mheshimiwa Bulaya najua kwamba Mbunge wa Jimbo ameshaniuliza mara kadhaa pia. Namuahidi tu kwamba pale Bunda eneo kilipo Kituo cha Polisi ni eneo dogo, limebanwa na barabara, kupitia jukwaa hili, nauomba uongozi wa Wilaya ya Bunda wapate eneo la kutosha kwa ajili ya kuweka mpango wa ujenzi wa Kituo cha Polisi cha hadhi ya Wilaya, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge sasa aulize swali lake.

Na. 139

**Kuwapatia wananchi Vitambulisho vya Taifa**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itamaliza kazi ya kuwapatia wananchi Vitambulisho vya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuwapatia wananchi Vitambulisho vya Taifa ni endelevu kwa kuwa kila mwaka kuna wananchi wanaotimiza umri wa miaka 18 ambao wanastahili kupewa Vitambulisho vya Taifa. Aidha, wapo wananchi wanaopoteza vitambulisho au wenye vitambulisho vinavyoharibika na hivyo kuhitajika vingine.

Mheshimiwa Spika, wananchi ambao walitambuliwa lakini hawajapata vitambulisho vyao, Serikali inatarajia kuwapatia vitambulisho vyao ifikapo mwezi Machi, 2024, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwa miaka 14 tangu *NIDA* ianze kazi, pale Sikonge waliopatiwa vitambulisho ni watu 61,000 tu kati 91,000 ambao walipigwa picha, maana yake ni kwamba kuna watu 30,000 hawajapatiwa vitambulisho, sasa nina maswali mawili ya nyogeza.

Je, Serikali ina mkakati gani katika kipindi cha miezi sita itawapatia vitambulisho watu wengi hivyo 30,000, wakati wastani kwa mwaka imekuwa ni 4,300? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa bado tuna watu karibu 60,000 hawajapigwa hata picha na siku hizi kuna masharti, ukienda leseni unaambiwa sharti la *NIDA* na huduma nyingine.

Je, kwanini Serikali haioni umuhimu wa kuahirisha hayo masharti mengine ili wananchi wasiendelee kudaiwa kitambulisho cha *NIDA* wakati haiwezekani kupata? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawakumbusha tena, leo ni siku yetu ya mwisho, msiongee na simu Bungeni; msiongee na simu Bungeni, yaani mnalifanya hili Bunge, hata hao watu wanaokuja kujifunza sijui wanajifunza nini kutoka kwenu. Kila mtu akishikilia simu namna hii unasikiliza saa ngapi majibu, unasikiliza saa ngapi

maswali? Milango iko sita, narudia tena milango iko sita, kama lazima uzungumze na simu, nenda nje. Usizungumze na simu Bungeni, ukizungumza tena usiseme mwalimu ameanza, nitakutaja ili utoke nje, ukazungumze huko nje. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kuhusu swali la kwanza, uhakika ndani ya miezi sita kwamba tutakamilisha upatikanaji wa vitambulisho kwa wananchi ambao hawajapata, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kwamba katika utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa nadhani Wabunge wote mnafahamu kwamba kwa miaka karibu mitatu hadi minne, mkataba ulikuwa umekuwa *frustrated* kwa sababu mkandarasi alikuwa anadai muda mrefu na madai yake yalikuwa hayajalipwa. Kwa dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tatizo lile amelikwamua, ametoa fedha tukalipa madeni tuliyokuwa tunadaiwa na uzalishaji wa vitambulisho umeanza.

Mheshimiwa Spika, tulichofanya kama Wizara ni kumsisitiza mkandarasi, kwa sababu kuna wananchi wengi walikuwa wanasubiri vitambulisho hivi, awe na mpango wa kasi wa kuzalisha na namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani aliniruhusu nikaenda mpaka kwenye kiwanda, nimejiridhisha kuwa uzalishaji unaenda kwa kasi kubwa. Ndiyo maana tuna uhakika kwamba ifikapo Machi, wananchi wote ambao walikuwa hawajapata vitambulisho watapata vitambulisho hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nimwondoe mashaka Mheshimiwa Mbunge. Tumeanza kuimarisha utendaji wa *NIDA*. Baada ya uzalishaji wa vitambulisho kuanza, *NIDA* imepanua uwezo wake kwa kuazima *staff* kutoka kwenye vyombo vyetu vingine vya usalama ili kuongeza kasi ya kuwafikiwa wananchi, waweze kupata zile namba za utambulisho.

Kwa hiyo, badala ya kusitisha zoezi zile, ngoja liendelee lakini tutaongeza idadi ya watu ili wananchi wako wa Sikonge ambao hawajapigwa picha na kupewa namba za utambulisho waweze kufanyiwa hivyo, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 140

**Marekebisho ya Sheria za Uvuvi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya marekebisho ya sheria zisizo rafiki kwa wavuvi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali imepanga kuendelea kupitia na kufanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 ili kukidhi mahitaji ya hali halisi ya sasa ya shughuli za uvuvi. Aidha, Serikali ina utaratibu wa kufanya maboresho ya kanuni mbalimbali za uvuvi mara kwa mara ili kuondoa kero na kuboresha mazingira ya biashara kwa wadau wa uvuvi. Kwa mfano, katika mwaka 2019 Serikali ilirekebisha kanuni kuruhusu leseni ya uvuvi iliyokatwa kwenye Wilaya moja kutumika katika Wilaya zote katika ziwa husika au ukanda wote wa bahari. Pia mwaka 2020

Serikali ilirejelea kanuni za uvuvi kuruhusu ongezeko la kina cha nyavu za makila katika Ziwa Victoria kutoka macho 26 mpaka macho 78 kwa uvuvi wa samaki aina ya sangara.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na tathmini ya sheria, kanuni, na miongozo iliyopo katika sekta ya uvuvi ili kubaini sheria zisizo rafiki kwa wavuvi nchini na kuzifuta au kuzirekebisha. Aidha, Wizara yangu iko tayari kupokea maoni na ushauri wa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge juu ya sheria zetu zinazohitaji kufanyiwa maboresho, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini tathmini hiyo itakamilika ili Watanzania wafanye kazi zao kwa ufasaha ili kuleta tija? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, kwa kuchelewesha kukamilisha taratibu hizo hatuoni kwamba tunawanyima Watanzania fursa katika kumiliki rasilimali zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba mchakato wa kubadilisha sheria ama kanuni ni mchakato unaofanyika mara kwa mara. Kama nilivyosema mwaka 2019 mchakato huo ulifanyika tukabadilisha sheria mbalimbali, mwaka 2020 tukabadilisha. Kwa hiyo, sheria ambazo zinaonekana pengine ni kandamizi kwa wadau wa uvuvi, Serikali iko tayari kuendelea kuzibadilisha mara kwa mara kadri ya mahitaji.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tathmini zinaendelea kulingana na sheria, jiografia na uhitaji wa maeneo husika. Lengo la Serikali hasa ni kuhakikisha kwamba sheria

zinazotumika kumsaidia huyu mvuvi ama mtumizi wa sekta hiyo kurahisisha shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tathmini zinaendelea. Sheria ambazo ni kinzani na mahitaji ya watumiaji wetu, zinaendelea kubadilishwa siku hadi siku kama ambavyo zimekuwa zikibadilishwa mara kwa mara. Kwa hiyo, wataalamu wanaendele kufanya tathmini, lakini sio tu wataalam wa Wizara, ni pamoja na watumiaji wa sheria hizi wanaendelea kufanya tathmini siku hadi siku kama ambavyo sheria na kanuni zimekuwa zikibadilika, naomba kuwasilisha. *(Mkofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninaleta matangazo niliyo nayo kabla hatujaendelea na ratiba yetu.

Kwanza, ni tangazo linalohusu wageni walioko hapa Bungeni; tunao wageni walio Jukwaa la Spika, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Katibu wa Kata ya Jangwani, Wilaya ya Ilala Jijini Dar es Salaam, Ndugu Riziki Kizingiti, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali na tutaanza na wageni 35 wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambao ni viongozi wa CCM na Wajumbe Kamati za Siasa za Holili, Ngoyoni na Nanjara kutoka Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, ambao ni wafanyakazi wa *AZAM TV* na Waratibu wa Kampeni ya Mito ni Maisha Yetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 51 wa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pauline Gekul ambao ni Wanafunzi wa hule ya Sekondari Hayatul kutoka Babati Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Ravia Faina ambao ni Diwani na Wajumbe kutoka Wilaya ya Kusini Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambaye ni Mbunifu wa Mavazi kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Wilago, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ighondo ambaye ni mpiga kura wake kutoka Singida Kaskazini, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni familia yake kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro, wakiongozwa na baba yake mzazi, Mzee Jacob Tarimo, karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wafanyakazi wa *Lerai Dry Cleaner* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni wanafunzi wenzake waliosoma pamoja Shule ya Sekondari *Kibondo Girls,* karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 67 wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni wamama watumishi wa Kanisa la Pentekoste kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni wifi yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambaye ni mpiga kura wake kutoka Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Salome Makamba ambao ni wanafunzi wa *Ruaha Catholic University* kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni 42, ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi na hawa ni Madiwani, Umoja wa Wanawake Tanzania na Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kata ya Migoli, Halmashauri ya Iringa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine yatawajia baada ya hii ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo kumi kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Laws updated with some challenges observed in its implementation)***
*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria zipatazo Ishirini na Tatu kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Legal Sector Laws in order to keep the laws updated with some challenges observed in its implementation)***
*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, miswada hii miwili imeshasomwa kwa mara ya kwanza, tunao Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2023* na Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Sekta ya Sheria wa mwaka 2023 *(The Legal Sector Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2023),* imesomwa kwa mara ya kwanza leo Bungeni, tarehe 8 Septemba, 2023.

Mara baada ya hatua hiyo, kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 97(1) ya Kanuni zetu za Bunge naelekeza miswada hiyo ifanyiwe kazi na Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu kwa taarifa hiyo muhimu.

Waheshimiwa tunaendelea na ratiba yetu baada ya kumsikia Katibu.

Haya, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**SPIKA:** Hoja ya kuahirisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, leo tunapoelekea kuhitimisha Shughuli za Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunayo kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukamilisha shughuli za Mkutano huu kama zilivyopangwa. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu, azidi kutukirimia hekima na nguvu katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ili tuweze kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru sana wewe kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge hili tukufu, hususani Mkutano huu wa Kumi na Mbili utakaohitimishwa hivi punde. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu, watakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Spika, ameendelea kuliongoza Bunge hili kwa busara na weledi wa hali ya juu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Naibu Spika, kwa kazi yake nzuri aliyoifanya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika, kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge lako. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile ambaye hivi karibuni ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wezangu, kwa michango, maoni na ushauri wakati wa mijadala na hoja mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa Mkutano huu. Michango yenu ni muhimu sana, kwani imekuwa ikisaidia Serikali katika utekelezaji wa mipango yake, hususani katika kutoa huduma kwa wananchi. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inathamini michango yenu, tumeipokea na niwaahidi kuwa tunakwenda kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka katika hatua nyingine ya kuimarisha utendaji ndani ya Serikali, tarehe 30 Agosti, 2023, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri. Kutokana na mabadiliko hayo, kipekee nianze na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu, anayeshughulikia uratibu wa shughuli za Serikali na Waziri wa Nishati, hongera sana. Kwa mara nyingine kwa niaba ya Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, tunakukaribisha na tupo tayari kukupa ushirikiano unaohitajika ili uweze kutekeleza majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze sana Mheshimiwa Jerry William Silaa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Uchukuzi; Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi; na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Naibu Mawaziri walioteuliwa, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi; nimpongeze vilevile Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi; nampongeza vilevile Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile aliyekuwa Mwenyekiti wetu wa Bunge, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi; na niendelee

kumpongeza pia Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati; na nimpongeze sana Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya uteuzi wa Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Waziri, Mheshimiwa Rais, alifanya mabadiliko ya baadhi ya Mawaziri na Manaibu Waziri, pamoja na kufanya uteuzi wa Makatibu Wakuu, Waheshimiwa Majaji na Mabalozi. Nitumie fursa hii kuwapongeza Viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na kuwatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwatake Viongozi wote walioteuliwa kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Viongozi wetu Wakuu, kufanya kazi kwa weledi, kuimarisha uhusiano mwema, uzalendo na kutanguliza kwanza maslahi ya Taifa letu. Kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alivyosisitiza kila mmoja akakiishi kiapo chake na kujituma katika dhamana aliyopewa ili kuleta mabadiliko tarajiwa. Vilevile zingatieni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano ulioanza 2021/2022 mpaka 2025/2026, lakini kuna Sheria, Sera, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, salamu za pole; mnamo tarehe Mosi Julai, 2023, Bunge lako Tukufu lilipata pigo la kuondokewa na Mbunge mwezetu, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mkoani Mbeya. Nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwako wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuondokewa na mwezetu, hakika atakumbukwa kwa busara zake na michango yake katika mijadala na hoja mbalimbali zilizowasilishwa hapa Bungeni. Nitoe pole kwa Wana-CCM wote, wanafamilia, ndugu na jamaa, marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wetu na tuendelee kumwombea Mwenyezi Mungu ampumzishe kwa amani na kumpa raha ya milele.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu wote waliopatwa na majanga mbalimbali yaliyosababishwa na majeruhi, uharibifu wa mali na kuondokewa na wapendwa wao. Kwa wale majeruhi tuendelee kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuimarisha afya zao ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Bunge, jumla ya maswali 140 ya msingi na mengine 504 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Pia jumla ya maswali saba ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na yalijibiwa. Niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuweza kujikita katika masuala mahususi yanayowahusu wananchi na maendeleo ya nchi yetu kupitia maswali mliyoyauliza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili taarifa moja, ambayo ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Kumi na Moja wa Bunge pamoja na utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo mbalimbali katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifanyia kazi taarifa kuhusu changamoto ya utekelezaji wa Mkataba wa Mauziano wa Matrekta ya Kampuni ya *URSUS* kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* na Wakulima. Kutokana na taarifa hiyo kupitia Bunge lako Tukufu ulitoa maelekezo kwa Serikali kufanyia kazi taarifa husika. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itafanyia kazi maelekezo yote kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, pia katika Mkutano huu Bunge lako Tukufu limepokea Miswada mitatu ya Sheria kama ifuatavyo:-

(1) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous*

*Amendments) (No.2) Bill, 2023);* muswada ulisomwa kwa hatua zake zote.

(2) Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa mwaka 2023; muswada ulisomwa katika hatua zake zote.

(3) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2023 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2023);* muswada huu uliwasilishwa kwa Hati ya Dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 107 hadi 112 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa kuzingatia wajibu wa Bunge. Bunge lako tukufu lilipokea kujadili na kupitisha Maazimio mawili kama ifuatavyo:-

(1) Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Katiba ya Tume ya Usafiri wa Anga ya Afrika ya mwaka 2009 *(The Constitution of the Africa Civil Aviation Commission, 2009);* na

(2) Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade and Services, 2012)*.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupokea, kujadili na hatimaye kuyapitisha Maazimio hayo. Weledi huu wa Waheshimiwa Wabunge unadhihirisha namna Bunge lako Tukufu lilivyosheheni wabobezi wa masuala mbalimbali yanayokusudia kupeleka mbele maendeleo ya nchi yetu na watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa ya Sekta ya Kilimo, hasa mwelekeo wa mvua za vuli na msimu wa kilimo mwaka huu wa 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka kuwa tarehe 24/8/2023 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilitoa utabiri kuhusu mwelekeo wa mvua za vuli kwa mwaka huu wa 2023. Utabiri huo unaonyesha uwezekano wa kunyesha mvua kubwa kuanzia Oktoba, 2023, ambapo mvua hizo zitanyesha kwa kiwango cha wastani wa juu na wastani wa kati katika baadhi ya maeneo. Maeneo yanayotarajiwa kuwa na mvua hizo ni pamoja na Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kigoma. Mikoa mingine ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Dar es Salaam, Pwani na Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho cha mvua kitawezesha uzalishaji wa kuridhisha wa mazao ya chakula. Hata hivyo, kuna uwezekano wa mvua hizo kuleta athari katika baadhi ya maeneo kama vile mafuriko, mmomonyoko wa udongo, pamoja na uharibifu wa miundombinu ya uzalishaji wa mazao. Ili kuhakikisha mvua hizo zinatumika vizuri na zinaleta tija katika uzalishaji, wakulima wanashauriwa kuzingatia yafuatayo:-

(1) Kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo kwa wakati ili kuongeza uzalishaji;

(2) Kufuatilia kwa ukaribu zaidi taarifa za mara kwa mara kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa ya hapa nchini; na

(3) Kuwasiliana kwa ukaribu na kufuata ushauri wa Maafisa Ugani waliopo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie upatikanaji wa pembejeo. Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa pembejeo hapa nchini ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Sote tunafahamu kuwa tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo hutegemea sana teknolojia ya kilimo, utaalam na upatikanaji wa pembejeo bora ikiwemo mbolea.

Mheshimiwa Spika, katika msimu huu wa kilimo 2022/2023, matumizi ya mbolea yaliongezeka kutoka tani 363,599 hadi tani

538,000, sawa na ongezeko la asilimia 48. Ongezeko hili linatokana na upatikanaji wa mbolea ruzuku, ambayo Serikali imekuwa ikitoa kuanzia msimu wa kilimo 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbolea nchini unaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko la matumizi ya mbolea limeenda sambamba na ongezeko la uzalishaji, hususan mazao ya chakula ambapo upatikanaji wa chakula sasa umeongezeka hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya mahitaji ya mbolea kwa msimu wa kilimo 2023/2024 ni tani 849,219. Hadi kufikia tarehe 31/8/2023 upatikanaji wa mbolea umefikia tani 480,622, sawa na asilimia 56.6 ya wastani wa mahitaji ya mwaka. Katika msimu huu wa kilimo, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima ili kuwapunguzia makali ya bei ya pembejeo hii muhimu katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, hivyo nielekeze sasa Wizara ya Kilimo kusimamia kikamilifu ugawaji wa mbolea yenyewe kwa wakulima ikiwemo kuongeza vituo vya mauzo ya mbolea na kuboresha mfumo wa upatikanaji wa mbolea hiyo kwa wakulima pamoja na kuvisogeza vituo hivyo karibu na wananchi kwenye maeneo yao ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie hali ya masoko ya mazao yaliyovunwa msimu wa 2022/2023. Katika kuhakikisha kuwa mazao yaliyovunwa katika msimu huu wa 2022/2023 yanapata soko la uhakika, bei nzuri na nchi kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imepanga kununua tani 305,000 za nafaka.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 5/9/2023, jumla ya tani 175,000 za nafaka sawa na asilimia 57 za lengo zimeshanunuliwa kupitia katika vituo 75 vilivyopo katika Kanda Nane za *NFRA*. Nitumie nafasi hii kuielekeza Wizara ya Kilimo tena kupitia *NFRA* kuimarisha miundombinu ya uhifadhi ili kuepuka kupoteza mazao ya chakula yanayoendelea kununuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2022/2023, bei za mazao mengine ya biashara zimeendelea kuimarika hususan mazao yanayotumia mfumo wa stakabadhi ghalani. Mathalani zao la kakao linalolimwa kwa wingi Wilaya ya Kyela na Mvomero, bei imefikia Sh.8,700 kwa kilo ukilinganisha na bei ya awali ya Sh.2,500. Kwa upande wa mbaazi, bei imeongezeka kutoka shilingi 1,500 kwa kilo hadi shilingi 2,200 kwa kilo katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi, lakini pia Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei ya ufuta imeongezeka vilevile na kufikia shilingi 4,000 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya awali ya shilingi 1,000 mpaka shilingi 1,200 kwa kilo msimu uliopita. Nitoe wito kwa wakulima nchini waendelee kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mazao haya kwa sababu tumeanza kuona tija ya bei nzuri inayopatikana. Hivi karibuni kulionekana *video* kutoka Wilaya ya Nanyumbu, wananchi wakicheza ngoma wakisherekea kupatikana kwa bei nzuri ya zao hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 7 Septemba, 2023 hapa nchini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amehitimisha Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Duniani lililofanyika Jijini Dar es Salaam *(AGRFA)* ambako nilimejadili na kuangalia mifumo ya kilimo na namna nchi itakavyoweza kunufaika, kumudu kujiongezea uwezo wa kuwa na chakula cha kutosha na ziada. Kupitia Jukwaa hilo lilibainisha fursa zitokanazo na kilimo, mijadala hiyo ilihusisha pia fursa pia fursa zilizopo kwenye sekta za mifungo na uvuvi katika kutoa fursa za kiuchumi kwa ujumla.

Mheshimwa Spika, Jukwaa hili kwetu limeleta manufaa makubwa, limekutanisha wataalam mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuweza kupeana uzoefu wa namna upatikanaji wa chakula cha kutosha katika kila nchi, nasi Tanzania tumejikita kwenye eneo hili katika kuhakikisha kwamba jamii yetu inapata chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie masuala ya usalama na afya kazini. Sambamba na kuimarisha sekta ya kilimo Serikali imeendelea kutekeleza adhima yake yakujenga mazingira bora ya kazi na wafanyakazi. Vilevile imeendelea kuhakikisha wafanyakazi wanapata stahili zao, vitendea kazi, kufatilia kwa ukaribu masuala ya afya na usalama mahala pa kazi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba masuala ya afya na usalama kazini ni haki ya msingi ya mfanyakazi na inapaswa kusimamia kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa nchi yetu imepiga hatua kubwa katika kusimamia masuala ya afya na usalama mahali pa kazi, kupitia taasisi yetu ya OSHA ambayo ina jukumu kubwa la kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 OSHA imefanya ukaguzi katika maeneo ya kazi 20,067 ukaguzi huo ni wa usalama wa umeme, mitambo ya kuzalisha mvuke, mitungi ya gesi na hewa, majengo na majenzi, eginomia, zana za kunyanyullia vitu vizito na vipimo vya ubora wa mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kaguzi hizo, taasisi yetu ya OSHA imeweshesha maeneo ya kazi kusimika mifumo ya kupunguza ajali, magonjwa na vifo vinavyotokana na mazingira ya kazi. Pia, imesajili maeneo ya kazi 11,036 na kuhamasisha wafanyakazi kupima afya zao kulingana na vihatarishi vilivyomo kwenye maeneo yao ya kazi, lakini pia utoaji wa elimu kwa waajiri na wafanyakazi, kusimamia viwango vya kazi pamoja na masuala ya afya na usalama wa kazi mahala pa kazi. Lengo hapa ni kuhakikisha kwamba sheria ya usalama mahala pa kazi inatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, kutokana na mafanikio ya taasisi yetu ya OSHA nchi mbalimbali zimekuwa zikija hapa Tanzania kujifunza kutoka kwa kwetu, baadhi ya nchi hizo ni pamoja na Zimbabwe, Botswana na Kenya. Aidha, hivi karibuni tumepokea maombi ya ugeni kutoka Eswatini na Afrika Kusini, watakaokuja kujifunza hapa kwetu masuala mbalimbali ikiwemo na mfumo wa TEHAMA wa usimamizi wa taarifa za kaguzi nchi *Work Place Inspection Management System - (WIMS),* ambayo pia na sisi tumeanza kuutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kujivunia pia kuona kuwa wataalum wetu kutoka taasisi yetu ya OSHA ndiye anayesimamia dawati la masuala ya afya na usalama mahala pa kazi katika Ofisi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* ambazo zipo Gaborone, nchini Botswana. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu kutoa mtaalamu kutoka ndani ya nchi kwenda nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Agosti, 2023, nilipata fursa ya kuwa Mgeni Rasmi kwenye hafla ya kugawa vitendea kazi na magarai 30, ambapo magari 17 ni ya Ofisi za Mikoa za Idara ya Kazi na 13 ni kwa ajili ya Taasisi ya OSHA. Magari hayo pamoja na vifaa vya kupimia afya na usalama mahali pa kazi vilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 4.3 na vilitolewa ili kuboresha utendaji kazi wa watumiaji au watumishi wa ofisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magari hayo 30 yalinunuliwa kwa fedha za ndani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alizozitoa katika Maadhimisho ya Sherehe za Mei Mosi, 2023 zilizofanyika Kitaifa Mkoani Morogoro. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutekeleza ahadi yake ndani ya kipindi kifupi sana na ninasisitiza watendaji wote kuongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku pamoja na kuimarisha usimamizi wa sheria ya usalama wa afya mahali pa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi. Pamoja na jitihada za Serikali kuimarisha usalama wa afya mahali pa kazi, Serikali inaendesha Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi ambao ni Taasissi ya Hifadhi ya Jamii iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha Tano cha Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Sura 263, kwa lengo la kulipa fidia wafanyakazi wanaopata ulemavu au kufariki kutokana na magonjwa au ajali zitokanazo na kazi.

Mheshimiwa Spika, kama yalivyo madhumuni ya kuanzishwa kwake Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi umeendelea kutekeleza kwa ufanisi jukumu la kulipa fidai kwa wafanyakazi hasa waliopata ajali ama magonjwa yanayaotokana na kazi. Aidha, mfuko unalipa fidia kwa wategemezi wao pale ambapo mfanyakazi anafariki kutokana na ajali mahali pa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa fidia umeongezeka kutoka shilingi bilioni 13.19 zilizolipwa kwa mwaka katika kipindi kilichoishia Juni, 2021 na kufikia shilingi bilioni 17.93 kwa mwaka kupitia kipindi kilichoishia Juni, 2023. Ongezeko hili linaufanya mfuko wa fidia kwa wafanyakazi kuwa umelipa jumla ya shilingi bilioni 62.04, kwa wanufaika 11,587 tangu ulipoanza kulipa fidia Julai, 2016 hadi ilipofikia Juni, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na malipo haya tathmini ya uhai wa uendelevu wa mfuko uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani kwa kipindi cha kuishia tarehe 30 Juni 2022, imeonesha kuwa mfuko ni endelevu na uko imara. Aidha, kwa mujibu wa hesabu ambayo zimewasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali kwa ajilI ya ukaguzi hadi tarehe 30 Juni, 2023 thamani ya mfuko imeongezeka na kufikia shilingi bilioni 665. 06. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi hasa udhibiti wa mfumo wa bei. Serikali imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei ambapo hadi kufikia Julai 2023, mfumuko wa bei umeendelea kupungua kwa kiasi na kufikia asilimia 3.3 kutoka asilimia 4.5 ya Julai, 2022. Kutokana na jitihada madhubuti za usimamizi wa fedha ni matarajio yetu kwamba mfumuko wa bei utaendelea kupungua na kubaki ndani

ya lengo hasa ikizingatiwa kuwa upatikanaji wa chakula nchini unazidi kuimarika, lakini bei nazo bado hazijatengamaa kikamilifu na Tanzania inaendelea kuwa na mfumuko wa bei wa chini ikilinganishwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Maelezo haya yanatokana na ulinganifu uliolinganishwa uliotokana na nchi za Jirani.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba Serikali inafikia azma ya utekelezaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi na ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimkakati, Serikali imeendelea kuongeza maarifa na matumizi ya teknolojia na mifumo ya TEHAMA kwenye ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilikusanya shilingi bilioni 26,241.8 sawa na asilimia 93.7 ya lengo ikilinganishwa na shilingi bilioni 24,396 ya mwaka 2021/2022. Kati ya kiasi kilichokusanywa mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 21,411.4 sawa na asilimia 95.6 ya lengo, na makusanyo yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 3,843.5 sawa na asilimia 83.5 ya lengo na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yalikuwa bilioni 984.9 sawa na asilimia 97.3 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zilizofanyika katika kuziba mianya ya upotevu wa mapato, bado kuna changamoto kadhaa ikiwemo ubadhilifu kutoka kwa watumishi wasio waaminifu, kutosomana kwa baadhi ya mifumo na kutokuwa na mifumo imara ya TEHAMA katika baadhi ya taasisi. Kutokana na changamoto hizo za kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali imeendelea kutekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchi katika sekta za uzalishaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi.

(ii) Kutambua na kusajili biashara zisizo rasmi na zinazoendeshwa kidigitali ili kutanua wigo wa mapato.

(iii) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kuongeza ulipaji kodi kwa hiari.

(iv) Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.

(v) Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ujulikanao kama TAUSI ili kupunguza urasimu uliokuwepo kwenye ukusanyaji wa mapato. Mfumo huu mpya ni wa kidigitali na utamrahisishia mfanyabiashara kufanya malipo ya Halmashauri kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu yake tu ya kiganjani au kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unalenga kumsadia mteja kujihudumia yeye mwenyewe, hali ambayo haimlazimu tena kwenda kwenye Halmashauri kuomba au kulipa tozo, ushuru, leseni, faini na vibali mbalimbali anavyovihitaji badala yake anaweza kufanya mwenyewe kupitia dirisha la mteja au *Tax Payer's Portal*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati kadhaa katika kudhibiti upotevu wa makusanyo ya ndani kwa kutumia mashine za kukusanyia ankara za mapato *(POS)*, ili kufikia azma hiyo Serikali ilisimika mfumo wa ulioboreshwa na ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Halmashauri zote nchi ujulikanoa kama TAUSI.

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe watumishi wa umma kuwa bado tunalo jukumu la kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kama Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt, Samia Suluhu Hassan, alivyosisitiza juu ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa wakati akifunga mafunzo ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala, pale Kibaha Mkoani Pwani, aliweka msisitizo bayana juu ya usimamizi wa makusanyo kwenye Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nawaelekeza wataalumu wetu wa ndani na wa mifumo ya TEHAMA wabuni programu tumizi za kuweza kutambua risiti halali na zilie ambazo siyo halali ili kuweza kujihakikishia kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingia Serikalini, vilevile waweke utaratibu wa kufanya kaguzi za kushtukiza kwenye mashine zetu za *POS* ili kubaini kama kuna ukiukwaji wowote unafanyika sambamba na kuwa na utaratibu endelevu waufuatilaji wa mfumo wa usalama maalumu wa utunzaji wa taarifa *backup*.

Mheshimiwa Spika, wakati naelekea kuhitimisha hotuba yangu naomba sasa nisisitize masuala muhimu yafuatayo: -

(i) Waajiri wachuke hatua za kuimarisha mifumo ya kuwalinda wafanyakazi wao dhidi ya vihatarishi vilivyopo katika maeneo yao ya kazi. Hatua hizo ni pamoja na kuwa na mwongozo wa usalama wa afya mahali pa kazi, kufanya tathmini ya vihatarishi mahali pa kazi, kuhakikisha wafanyakazi wao wanapimwa afya ili kubaini athari ya vihatarishi kwa wafanyakazi na kuhakikisha maeneo yao yanafanyiwa kaguzi za usalama wa afya ili kuwalinda wafanyakazi na kulinda uwekezaji wao. Aidha, nitoe wito kwa watumishi wa OSHA wawe waadilifu wanaopenda kuendesha mazoezi ya ukaguzi wa mara kwa mara mahali pa kazi na kuchukua vipimo vya wafanyakazi.

(ii) Wafanyakazi wahakikishe wanazingatia taratibu na miongozo ya kujilinda dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kusababisha ajali au magonjwa wanapokuwa nawatekeleza majukumu. Hii itasaidaia sana kulinda afya na usalama wao pamoja na kumpunguzia mwaajiri gharama za uendeshaji pale anapougua au kupata ajali mtumishi wake anapokuwa kazini.

(iii) Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi uongeze wigo wa kutoa elimu kwa wafanyakazi ili watambue huduma zinazotolewa na mfuko huo, lakini vilevile waajiri watumie ipasavyo mifumo ya TEHAMA kupata huduma, kujisajili na kuwasilisha kwa wakati michango katika mfuko huo.

(iv) Napenda kuwasisitiza wafanyabiashara na watoa huduma watoe risiti halali kupitia mashine za elektroniki, wakati wa mauziano ya bidhaa au utoaji wa huduma kwa wateja, kwa upande wa wateja niwakumbushe kuwa ni wajibu wao kudai risiti yenye thamani halisi ya fedha ulizotoa.

(v) Maafisa Masuuli waimarishe usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na kutekeleza kikamilifu mpango wa bajeti ya mwaka 2023/2024.

(vi) Watendaji wote Serikali imarisheni ukusanyaji wa mapato na kufanya matumizi kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Bajeti sambamba na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

(vii) Watumishi wa Umma watenge muda wa kwenda kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika maeneo yao, wafuateni, wasikilizeni na kutatua kero zao ili wasipoteze muda mwingi kufuatilia. Pia, wasilazimike kwenda ngazi za juu au kusubiri ziara za Viongozi wa Kitaifa kwa masuala ambayo yangeweza kufanywa na watumishi kwenye ngazi husika. *(Makofi)*

(viii) Hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya watumishi wote wanaosababisha upotevu wa mapato ya Serikali na niwaelekeze Wakuu wa Mikoa kwa Mikoa yote kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kubaini wabadhilifu hao wachukuliwe hatua mara moja na kutoa taarifa kwa mamlaka zao za juu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo. Kwa upande wa michezo nchi yetu imeendelea kupata mafaniko makubwa sana. Sote tumeshuhudia vilabu vyetu viking'ara katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi, hivi karibuni tumeshuhudia Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 18, ikichukua ubingwa wa mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika Mashariki - *CECAFA* baada ya kuishinda timu ya Uganda kwa bao moja bila katika mchezo uliofanyika kwenye viwanja vya Azam Jijini Dar Es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia *JKT Queens* ambayo imefanikiwa kuchukua ubingwa wa *CECAFA* na hivyo kupata fursa ya kuwakilisha ukanda wa Afrika Mashariki na Kati katika mashindano ya vilabu vya Afrika. Ushindi wa timu hizi za mpira wa miguu za wanawake ni wa kujivunia sana. Nyote mtakubaliana nami kuwa Timu za wanawake kwa sasa zimehamasika na zinaendelea kufanya vizuri na kushinda kwa kasi ya juu. Nawatakia kila la heri *JKT Queens* katika mashindano yanayaofuata na nitoe wito kwa wapenzi wa michezo na Watanzania wote kwa ujumla, tuendelee kuwaunga mkono ili wazidi kupeperusha bendara ya nchi yetu. Niwasihi waendelee kujifua kwani ushidi ni lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuipongeza sana Timu ya Taifa ya soka ya ufukweni ambayo katika Mashindano ya Afrika *(African Games)* imeshika nafasi ya tatu na kupata medali ya shaba, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchezo wa ngumi ali maarufu masumbwi nawapongeza sana wanamasumbwi walioshiriki katika mashindano mbalimbali, kipekee nimpongeze Grace Mwakamele, aliyetunukiwa medali ya fedha, katika mashindano ya ngumi yaliyofanyika Yaounde nchi Kameruni, huyu ni mwanamke wa kwanza Mtanzania kushinda medani ya Kimataifa. Pia, nampongeza bondia Yusuf Changarawe, aliyatunukiwa medali ya shaba, katika mashindano hayo yaliyofanyika tarehe 25 Julai, hadi tarehe 6 Agosti, 2023, na nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaishukuru Serikali ya India kupitia Ubalozi wake hapa nchi pamoja na Taasisi ya Kalamandalang kwa kuwaunga mkono wachezaji wetu wa Tanzania kwani kwa miaka miwili mfululizo wamekuwa wakiwaanda katika hafla maalumu ya kuwapongeza na kuwapa zawadi washindi wetu, ona sasa nchi ya India inawapa zawadi washindi wetu, tuwapigie makofi hawa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia mashindano ya *Africa Open*, katika mchezo wa gofu yaliyofanyika nchini Ghana, mchezaji mwanadada shupavu Madina Iddi ameibuka bingwa wa mashindano hayo. Nitumie fursa hii kumpa pongezi sana Madina

Iddi, kwa ushindi huo mkubwa. Vilevile ninawapongeza wanawake wote wanaodhubutu kushiriki katika mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, jitihada zenu tunaziona na kwa hakika mmeendelea kuliheshimisha Taifa hili, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Michuano ya Klabu Bigwa ya Shirikisho Barani Afrika, napenda nizipongeze timu zetu za Yanga, Simba na *Singida Fountain Gate,* kwa kufanikiwa kuingia kwenye hatua ya pili ya mshindano hayo, hakika mmeanza vyema. Nitumie nafasi hii kuwatakia kila la heri katika mashindano yanayoendelea na yajao, mpate ushindi mnono na kuweza kuingia katika hatua ya makundi ili kutupa raha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niipongeze timu ya *Simba Sports Club* ambayo imekuwa miongoni mwa vilabu…. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie eneo hili kwa sababu kulikuwa na makofi mengi haijasikika vizuri. Kipekee naomba niipongeze timu ya *Simba Sports Club* ambayo imekuwa miongoni mwa Vilabu Nane Bora Barani Afrika ambavyo vitashiriki michuano ya *Africa Football League*. Michuano hiyo inatarajiwa kuzinduliwa mwezi Oktoba, 2023, Jijini Dar es Salaam. Niwasihi Watanzania kujitokeza kwa wingi kwenye ufunguzi wa michuano hiyo ambayo itafanyika hapa nchini, kwani kufanya hivyo inaitangaza Tanzania Kimataifa, hongera sana *Simba Sports Club*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, timu yetu ya Taifa au *Taifa Stars* jana ilishiriki katika mechi ya kufuzu kuwania Kombe la Mataifa ya Afrika *(Africa Cup of Nation 2024)* yatakayofanyika nchini Ivory Coast. Katika michuano hiyo Tanzania ilihitaji kushinda au kutoka sare ili kuweza kufuzu katika kundi lake. Ninayo furaha sana kuipongeza *Taifa Stars* kufuzu michuano ya kuwania kushiriki fainali za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kwenye eneo hili, ninayo furaha sana kuipongeza *Taifa Stars* kufuzu michuano ya kuwania kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika baada ya kupambana na Timu ya Taifa ya Algeria huko nchini Algeria. Katika mechi hiyo, timu yetu

ilitoka suluhu (bila bila) na kuifanya ipate tiketi ya kuendelea na mashindano hayo. Ninaipongeza sana timu yetu ya Taifa na kuitakia kila la heri katika mashindano yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwasihi Watanzania wenzangu, tuendelee kuunga mkono, kuiunga mkono timu yetu ya Taifa ili ipate hamasa zaidi ya kutuletea ushindi tunaoutarajia.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, ninapohitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Watendaji wa Serikali ambao wamekuwa chachu kubwa katika kutekeleza masuala ya kitaalam kwa weledi mkubwa kupitia mipango na ushauri katika kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza wajibu wake upasavyo hasa kwa kuishauri vyema Serikalli yetu katika kipindi chote cha mkutano huu. Ninamshukuru Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge kwa kuhakikisha wanatupatia huduma nzuri iliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee navishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi yao nzuri ya kuendelea kusimamia utulivu na amani katika kipindi chote cha Bunge. Nawashukuru sana wanahabari kwa kazi kubwa mliyoifanya ya kuwa habarisha wananchi yale yaliyokuwa yakijiri kwenye mkutano huu pamoja na madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni na tunategemea waturudishe kwenye maeneo yetu. Tuna imani Mwenyezi Mungu atatuongoza vyema mpaka kwenye maeneo yetu. Hongera sana, ninawashukuru sana madereva wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwatakie Waheshimiwa Wabunge wenzangu safari njema mnaporejea Majimboni kwenu. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape afya njema na nguvu za kutosha katika kutekeleza wajibu kwa kuwahudumia wananchi kwenye maeneo yetu au kwenye Majimbo yenu na maeneo ya uwakilishi mliopewa dhamana ya kuyaongoza.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kati ya Tarehe 27 au 28 mwezi huu wa Septemba mwaka huu wa 2023, kutegemea mwandamo wa mwezi. Kutakuwa na siku ya maulidi. Natumia fursa hii kuwatakia Waislamu wote na Watanzania wote kwa ujumla maadhimisho mema ya Mazaazi ya Mtume Mohamad *(S.A.W)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya niliyoyatoa kwenye sekta mbalimbali sasa ninapenda kutoa hoja kuwa, Bunge lako tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne tarehe 31 Oktoba, 2023 saa tatu kamili asubuhi tutakavyokutana tena katika ukumbi huu hapa mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Nawaona Wabunge watatu tu ndiyo hawajaunga mkono. Naona wanataka kubaki hapa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Tunaweza kuketi. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa hapa sasa waseme ndiyo. Waheshimiwa Wabunge, nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na mambo mengine aliyoyaeleza ni hoja ya kuliahirisha Bunge. Kwa hiyo, imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasema mengine naona kuna watu wameitikia siyo wasijue maana ya kusema siyo kwenye hoja kama hii maana yake ni nini. Jambo lolote linalotolewa kwenu kwa ajili ya maamuzi uwe umetafakari kabla haujaisema kura yako. Usiseme hapana kama ulikusudia kusema ndiyo na usisema ndiyo kama ulikusudia kusema hapana.

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni hapa. Kabla sijaleta tangazo la wageni natumia fursa hii kuwashukuru sana watumishi wote wa Bunge wakiongozwa na Katibu wetu wa Bunge kwa kazi nzuri walioifanya. Wameliwezesha Bunge hili kufanya kazi kwa ufanisi. Tunakushukuru sana Katibu wa Bunge pamoja na watumishi wote wa Bunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia natumia nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge wote kwa kazi nzuri mlioifanya na kulifanya Bunge letu liweze kufanya kazi ambazo tulipaswa kuzifanya katika kipindi hiki cha Bunge hili fupi la Mwezi wa Tisa. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano mlioutoa. *(Makofi)*

Pia ninawashukuru sana wasaidizi wangu kwa maana ya Wenyeviti wanaokaa hapa mbele, lakini pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika. Ninawashukuru sana kwa usaidizi wao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia ninaishukuru Serikali kwa ushirikiano ulioutoa, pamoja na mambo mengine Bunge linafanya shughuli nyingi za Serikali mkiongozwa humu Bungeni na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawashukuru kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya na kwa ushirikiano ambao mmeutoa kwa Bunge. Mtupelekee salamu hizo kwa Mheshimiwa Rais ambaye ndiye anaongoza Serikali kwa ushirikiano ambao ameendelea kuutoa kwa Bunge hili. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuwashukuru pia wananchi ambao wamelifuatilia Bunge lao kujua ni mambo gani yanayofanyika hapa.

Hiyo inawarahisishia kujua ni maeneo gani waendelee kuwatuma Wabunge wao waendelee kuwasemea humu ndani. Kwa hiyo, tunawashukuru pia wananchi wote wa Tanzania kwa kuendelea kulifuatilia Bunge lao katika mambo mbalimbali ambayo yanafanywa.

Pia tumekuwa tukisaidiwa hapa na *brass band* kufungua Bunge letu na kufunga. Leo wapo hapa. Tunawashukuru sana *Brass Band* kwa ushirikiano ambao umeendelea kuutoa na tunaamini mtaendelea kushirikiana nasi. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi hili la wageni ambalo ninataka kulitangaza sasa ndilo kundi la mwisho la wageni litakalokuwa linatangazwa la wageni kwa Bunge hili. Tunawashukuru wageni wote ambao wametembelea Bunge letu kuja kujifunza na kuona mambo namna yanavyofanyika. Hawa ninaowatangaza hapa ndiyo walioingia sasa, wengine tulikuwa tumeshawatangaza na wameshatoka Bungeni.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa David Kihenzile ambao wanaongozwa na Ndugu Richard Kasesela ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi 173 na walimu saba kutoka Shule ya Wavulana Tengeru na *Holly Ghost* - viziwi kutoka Tengeru Jijini Arusha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwatakia kila la kheri mnapoanza safari za kurejea Majimboni kwenu. Kila mmoja kwenye majukumu yake kwa sababu, wapo wanaoenda Majimboni na wapo wale ambao wanakwenda kwenye Shughuli mbalimbali za Bunge. Kwa hiyo, wananchi wasije wakasema wa kwetu hatajamuona hapa. Baadhi ya Wabunge wanakwenda kwenye shughuli za Kibunge lakini baadaye wataungana nanyi wananchi ili kuja kusikiliza mawazo yenu. Ninawatakia safari njema na kazi njema kila mmoja kule aelekeapo

na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu aturejeshe sote salama hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nimwite Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 31 Oktoba, 2023 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 5.54 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 31 Oktoba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*